




UKURASA 3

**KAMPUNI** simu Tigo, ZANTEL zauzwa rasmi





# Nipashe

Alhamisi Aprili 7, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580908

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


# Samia azidi kuibana MSD

**ATAKA** kuchunguzwa mfumo ufuatiliaji dawa, ni wiki baada ya kutangaza kusukwa upya... *Endelea Uk. 2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akibonyeza kitufe kuzindua mfumo wa usafirishaji wa dharura kwa wajawazito na watoto wachanga (M-MAMA), jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA 2

## Serikali yamwaga ajira 32,000 elimu na afya



## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### LATRA YAITA WADAU KUJADILI NAULI MPYA

WAKATI Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ikiwaita wadau wa usafiri ili kutoa maoni yao kuhusu mapendekezo ya viwango...

UKURASA WA 4

### AJITOSA BAHARINI NA KUFA AKIWAKIMBIA POLISI

MKAZI wa mtaa wa Sabasaba, Kata ya Jamhuri, Manispaa ya Lindi, Hassani Mussa M'buyu (27), amekufa maji, baada ya kujitosa baharini kwa madai ya kukimbia kukamatwa kwa tuhuma za kutishia kumuua mpenzi wake...

UKURASA WA 19

### BLAISE COMPAORÉ JELA MAISHA KWA MAUAJI YA THOMAS SANKARA

Rais wa zamani wa Burkina Faso, Blaise Compaoré amehukumiwa kifungo cha maisha jela, kwa kushiriki katika mauaji ya mtangulizi wake Thomas Sankara...

## W'biashara kikaangoni upandishaji bei bidhaa

UKURASA 3

**MICHEZO** MORRISON AITIA SIMBA HASIRA KWA ORLANDO UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

## Serikali yaridhia kulipa tril. 2.17/- za mafao

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali imeridhia kulipa deni la Sh. trilioni 2.17 katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) ambazo ni stahiki ya mafao kwa wanachama waliorithiwa kutoka uliokuwa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF) mwaka 1999.

Akiwasilisha bungeni jijini hapa jana hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi kwa ofisi yake kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema serikali iliridhia kulipa deni hilo huku akibainisha kuwa tayari PSSSF wamelipa mafao kwa wanufaika, wastaafu na wategemezi wapatao 32,467 yenye thamani ya Sh. trilioni 1.05 katika mwaka huu wa fedha.

Waziri Mkuu pia alisema kuwa mfuko pia umelipa Sh. bilioni 352.51 ambazo ni pensheni ya kila mwezi, sawa na wastani wa Sh. bilioni 58.75 kila mwezi kwa wastaafu 148,866.

MAFAO NSSF

Majaliwa alisema Shirika la Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) limelipa mafao kwa wanufaika, wastaafu na wategemezi 98,202 yenye thamani ya Sh. bilioni 363.7 na kuongeza kuwa mfuko pia umelipa Sh. bilioni 64.9 ikiwa ni pensheni ya kila mwezi kwa wastaafu 24,881.

"Katika kujenga mazingira wezeshi kwa waajiri na kupunguza gharama za uendeshaji, serikali kupitia Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) imepunguza kiwango cha uchangiaji kwa waajiri wa sekta binafsi kutoka asilimia moja (1) hadi asilimia 0.6.

"Uamuzi wa kupunguza kiwango hicho cha uchangiaji, umetokana na utekelezaji wa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu taasisi za serikali kuhakikisha zinaweka mazingira bora ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini ili kukuza uchumi wa nchi na kulinda rasilimali watu," alisema.

# Rais Samia azidi kuibana MSD

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameiagiza Wizara ya Afya kuchunguza haraka mifumo inayotumiwa na Bohari Kuu ya Dawa (MSD) hasa ufuatiliaji wa dawa tangu zinapotoka hadi pale zinapofika kwenye vituo.

Samia alitoa agizo hilo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza kwenye uzinduzi wa kitaifa wa mfumo wa usafirishaji wa dharura kwa wajawazito na watoto wachanga (m-mama).

Agizo hilo amelitoa ikiwa takriban ni wiki moja tangu alipoweka bayana kwamba taasisi hiyo inapaswa kusukwa upya ikiwa ni pamoja na kufumua uongozi mzima na kuweka watu wapya. Alisema hayo baada ya kupokea ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ambayo pamoja na mambo mengine, ilionyesha upungufu katika utendaji kwenye taasisi hiyo.

"Naomba niwaahidi Watanzania kutoa au kujenga kasi ya mfumo wa huduma bora za afya. Tumeanza kulifanyia kazi hilo kutoa huduma bora za afya kama alivyosema Waziri wa Afya (Ummy Mwalimu). Tumeanza na ujenzi wa miundombinu ambapo vituo kadhaa ngazi ya vijiji, kata, wilaya na ngazi za mikoa na kazi ya kununua na kusambaza vifaa tiba inaendelea.

"Upatikanaji wa dawa tumetoa mabilioni kwa ajili ya ununuzi wa dawa lakini kuna mapungufu (upungufu) na juzi nilipotoa agizo kwa wizara kuangalia masuala ya mifumo nilitoa pia agizo la kuiangalia MSD kwa haraka sana. Najua sehemu moja ni yangu na nakuahidi kwamba nitaifanya kwa haraka lakini kwenye mifumo ya kutoa huduma ni sehemu yako, naomba mkaifanyie kazi haraka sana na zaidi ule mtandao wa kuifuatilia dawa mpaka pale inapofika. Ukiharakishwa itakuwa vizuri zaidi," alisema.

Pia alisema serikali imejitahidi kuajiri watumishi katika sekta ya afya na kwa mwaka jana, watumishi 3,600 waliajiriwa.

"Na kwa mwaka huu uchumi wetu umeturuhusu kuajiri watumishi 32,000 ndani ya taifa letu ambao kati ya hizo nyingi zitakwenda katika sekta ya afya na elimu bila shaka" alisema.

Kadhalika alisema pamoja na kuanzishwa kwa mfumo huo wa m-mama serikali imehakikisha maeneo yote yanakuwa na magari ya kubeba wagonjwa angalau kila kata gari moja.

"Tumeagiza 'ambulance' (magari ya kubeba wagonjwa) 233 za kawaida ambazo zitamwagwa Tanzania nzima lakini pia tumeagiza 'ambulance' 25 ambazo ni 'advance' hizi ni kama ngazi ya rufani. Kama zile zinakuwa hazitoshi au hazina vifaa basi hizi 25 zitatumika lakini pia tumeagiza magari 242 ya uratibu ni matumaini yangu kwamba magari na 'ambulance' hizi zitakwenda kuongeza nguvu kwenye huu mpango wa m-mama ili kuwawahisha watoto na kinamama hospitalini," alisema.

Rais pia alisema kupitia Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) serikali katika mwaka wa fedha uliopita imetoa fedha nyingi ili kuboresha miundombinu ya barabara za vijijini na kurahisisha utoaji wa huduma za afya.

Rais Samia aliipongeza kampuni ya simu za mkoani ya Vodacom kwa kuwezesha mfumo huo wa m-mama ambao utasaidia kuratibu usafiri kwa ajili ya wajawazito na watoto wachanga kupitia magari ya kubeba wagonjwa yaliyosajiliwa na magari binafsi.

Waziri Ummy alimpongeza Rais Samia kwa jitihada ambazo amekuwa akizifanya katika kuboresha sekta ya afya kwa kutoa kiasi kikubwa cha fedha.

Ummy alisema hivi sasa wanapanga kufanya mazungumzo na Vodacom ili kutengeneza mfumo utakaosaidia kufuatilia usambazaji wa dawa kutoka MSD hadi katika vituo vya afya.

Alisema lengo la serikali ni kutekeleza mpango wa m-mama nchi nzima ili kukomesha vifo vya wajawazito na watoto wachanga.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Stanslaus Nyongo, alisema bunge litaendelea kuipa serikali ushirikiano katika kuwaletea wanachi maendeleo.



Rais Samia Suluhu Hassan akimsikiliza Mkurugenzi wa M-MAMA, Dolorosa Duncan (kulia), kuhusu mfumo wa usafirishaji wa dharura kwa wajawazito na watoto wachanga M-MAMA, kabla ya kuuzindua, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Serikali kumwaga ajira 32,000

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imesema wiki ijayo inatarajia kutangaza ajira za kada mbalimbali 32,000 ikiwamo za afya na elimu ili kukabiliana na upungufu uliopo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, ndiye aliyebainisha kuhusu hatua hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu maswali ya wabunge waliohoji mkakati wa serikali wa kuajiri watumishi hasa wa sekta ya elimu na afya.

Mhagama alisema: "Nimesikiliza maswali ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) wabunge wengi wakiuliza maswali ya nyongeza wamekuwa na hofu ya uhaba wa watumishi hasa sekta ya elimu na afya, nasimama hapa kwa heshima kubwa ya rais, naomba niwaarifu waheshimiwa wabunge, Mheshimiwa Rais na serikali yake wametambua tatizo la uhaba wa watumishi hasa kwenye miradi ya sekta ya afya na elimu."

Alisema Rais ametoa kibali cha kuajiri ambapo katika ahadi ya serikali kwa mwaka 2021/22 ilikuwa ni kuajiri watumishi 44,000.

"Tayari serikali ilishaajiri watumishi wapya na ajira mbadala 12,000, naomba niwathibitishie waheshimiwa wabunge Mheshimiwa Rais ameridhia na wiki ijayo itatoa tangazo refu la ajira 32,000 na utaratibu wa ajira hizo, na mgawanyo wake katika sekta ambazo zinaongoza kwa uhaba watumishi maelezo yote tutayatoa wiki ijayo."

"Kwa hiyo waheshimiwa wabunge naomba kuwahakikishia serikali ya awamu ya sita inajali tatizo la uhaba wa watumishi nchini,"alisema.

Mwenyekiti wa Bunge, David Kihenzile, alipongeza serikali kwa hatua hiyo kwa kuwa ni tatizo kubwa kwa watumishi.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Buyungu (CCM), Aloyce Kamamba, alihoji serikali ina mpango gani wa kupeleka Watumishi wa Afya wa Kada mbalimbali katika Wilaya ya Kakonko.

Pia katika swali la nyongeza, Mbunge wa Nkenge(CCM), Florent Kyombo, alisema vipo vituo vya afya vilivyojengwa na kukamilika bado havina watumishi wa kada ya afya wakutosha na kuhoji serikali ina mpango gani wa kuajiri.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), David Silinde, alisema katika mwaka wa fedha 2020/21 Serikali iliajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya 2,726 ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko ilipelekewa watumishi 24 waliopangwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Aidha alisema Serikali katika mwaka wa fedha 2021/22 imepanga kuajiri watumishi 7600 wa kada mbalimbali za afya kwa ajili ya kuboresha hali ya utoaji huduma za afya kote nchini ikiwemo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko.

Aidha, alisema serikali kwa kushirikiana na wadau itaendelea na mpango wa kuajiri watumishi wa kada za afya kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

HABARI KITAIFA

# Wafanyabiashara kikaangoni kwa upandaji bei ya bidhaa

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

SERIKALI imewataka wazalishaji na wasambazaji wa bidhaa muhimu kushusha mara moja bei za bidhaa walizopandisha pasipo kuendana na uhalisia wa soko.

Imesema kupaa kwa bei za bidhaa kumeshuhudiwa katika kipindi hiki cha mfungo wa Ramadhani na Kwaresma huku ikibainisha hatua mbalimbali ilizozichukua kukabiliana na hali hiyo.

Akiwasilisha bungeni jijini hapa jana hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi kwa ofisi yake kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alisema hivi karibuni kumekuwapo taarifa za uhaba na upandaji wa bei usioendana na uhalisia wa soko kwenye bidhaa za ujenzi, vyakula, nishati na pembejeo za kilimo.

Kutokana na hali hiyo, alielekeza Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kuunda jopo la wataalamu ili kufuatilia taarifa hizo.

Majaliwa alisema wizara hiyo kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Tume ya Ushindani (FCC), ilifanya ufuatiliaji na tathmini ya mwenendo wa bei za bidhaa muhimu zinazozalishwa nchini na zile zinazotumia malighafi kutoka nje ya nchi.

"Serikali imechukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na upandaji huo wa bidhaa muhimu. Hatua hizo ni pamoja na usimamiaji wa Sheria ya Ushindani Na. 8 ya Mwaka 2003 ambayo inazuia kupanga bei.

"Hatua nyingine ni serikali kutafuta vyanzo mbadala vya upatikanaji wa bidhaa na kuweka mifumo ya kusimamia masoko ya awali na minada.

"Serikali inawaelekeza wazalishaji na wasambazaji wa bidhaa muhimu kushusha mara moja bei za bidhaa walizopandisha pasipo kuendana na uhalisia wa soko ikiwa ni pamoja na kutotumia kipindi hiki cha mfungo wa Ramadhani na Kwaresma kupandisha bei.

"Nawasihi wazalishaji na wafanyabiashara wa bidhaa muhimu kuuza bidhaa husika kwa kuzingatia gharama halisi za uingizaji, uzalishaji na usambazaji. Wale watakaobainika kupandisha bei bidhaa muhimu bila utaratibu, hatua kali zitachukuliwa dhidi yao," alionya.

Waziri Mkuu alitaja maeneo mengine saba yatakayopewa kipaumbele na serikali katika mwaka ujao wa fedha kuwa ni pamoja na: Sensa ya Watu na Makazi iliyopangwa kufanyika Agosti. mwaka huu; kuvutia wawekezaji wakubwa; kudumisha amani na usalama nchini.

Alivitaja vipaumbele vingine ni: Wananchi kuwezeshwa kiuchumi; kukuza biashara na uwekezaji pamoja na kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza rasilimali watu; kukuza Sekta Binafsi pamoja na kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi; na kushirikiana kwa karibu na jumuiya za kimataifa katika kukabiliana na kutokomeza maambukizi ya virusi vya UVIKO-19.

Ili kutekeleza majukumu yake katika mwaka ujao wa fedha, Majaliwa aliliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 148.892 kwa ajili ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake. Kati yake, Sh. bilioni 101.365 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 47.527 ni kwa ajili matumizi ya maendeleo.

Pia aliliomba Bunge liidhinishe Sh, bilioni 132.729 kwa ajili ya Mfuko wa Bunge. Kati yake, Sh. bilioni 127.329 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 5.4 ni kwa ajili matumizi ya maendeleo.

## Kampuni za Tigo, Zantel kuuzwa rasmi

**Na Jenifer Gilla**

Kampuni ya huduma ya mawasiliano ya AXIAN kwa kushirikiana na Rostam Aziz zimetangaza kukamilika kwa mchakato wa umiliki wa kampuni za mitandao ya simu iliyounganishwa ya MIC Tanzania Public Limited Company (Tigo na Zantel).

Akizungumza na waandishi wa habari, jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa AXIAN Telecom, Hassanein Hirdjee, alisema mpango huo utaunganisha wateja milioni 14 wa simu za mkononi kwa AXIAN Telecom na kuharakisha ukuaji wa kampuni hizo barani Afrika ambapo kwa sasa imefika nchi nane.

Aliongeza kuwa mpango huo ni ukuaji na wenye matumaini wa muungano wa AXIAN Telecom unaojumuisha uwekezaji mkubwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kipindi cha miaka mitano ijayo, ili kuimarisha ubora wa huduma zitolewazo na kampuni iliyounganishwa ya MIC Tanzania PLC.

"Tunayo furaha kuanza safari hii ya kusisimua na wenzetu wa hapa (Tanzania) na ninaamini kwa pamoja tutafanikisha mambo makubwa yatakayoendelea kuongoza mapinduzi ya kidijitali nchini. Tunatoa shukrani zetu kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutusaidia kufanikisha mchakato huu, tunatarajia kuendelea kushirikiana kwa pamoja," alisema Hassanein.

Alisema muungano wa AXIAN Telecom umeweka vipaumbele vinne muhimu katika kutekeleza majukumu yake katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwamo kuendeleza mabadiliko ya kidijitali kwa kutumia teknolojia za kisasa na kutoa huduma zinazowanufaisha mtumiaji mmoja mmoja na makampuni ya Kitanzania.

Alitaja pia kuongeza upatikanaji wa huduma nafuu za mawasiliano na kuongoza ujumuishwaji wa kidijitali kwa kuwekeza kikamilifu kwenye ujenzi wa miondombinu ya mawasiliano kwa kuimarisha upatikanaji na ubora wa mtandao hasa kupitia teknolojia ya 4G.

Kipaumbele kingine alisema ni kuongeza kasi ya ujumuishwaji wa huduma za kifedha kwa njia ya simu za mkononi, kwa kuzingatia mafanikio ya huduma hizi kutoka kwenye kampuni zilizounganishwa ili kuendeleza zaidi huduma za kifedha kwa njia ya simu zinazolenga mahitaji ya wateja wa Tanzania.

Na mpango wa mwisho ni kukuza maendeleo ya taaluma za wafanyakazi na kuweka mkazo mkubwa kwenye mafunzo, kubadilishana uzoefu na kushirikishana maarifa ya pamoja miongoni mwa wafanyakazi wa kampuni iliyounganishwa ya MIC Tanzania PLC.

Mwenyekitii MIC Tanzania PLC, Rostam Aziz, alisema walipoanza safari ya mawasiliano zaidi ya miaka 20 iliyopita na AXIAN, lengo kubwa lilikuwa kuunganisha watanzania kwenye huduma hii. "Tulikuwa waanzilishi katika kujenga mtandao wa huduma za simu, hasa katika maeneo ya vijijini, ambapo kwa sasa Watanzania wenzangu wengi wanafurahia huduma hii. Tukitazama malengo ya pamoja na AXIAN," alisema Rostam.

Alisema kupitia muungano huo wataondoa vikwazo vinavyozuia upatikanaji wa huduma za kidigitali nchini kote, kwa kuzingatia mahitaji muhimu kwa Watanzania na kampuni.

AXIAN Telecom inatoa huduma ya mawasiliano barani Afrika katika masoko manane kupitia kampuni tanzu nchini Madagascar, Comoro, Reunion, Mayotte, Senegal, Togo, Uganda sasaTanzania.


## TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA

### TAARIFA YA UPANUZI WA MASHIMO YA GENA NA GOKONA YALIYO KATIKA MGODI WA DHAHABU WA NORTH MARA, WILAYA YA TARIME, MKOA WA MARA

Mradi pendekezwa wa upanuzi wa mashimo ya Gena na Gokona (Mradi) upo ndani ya Wilaya ya Tarime katika Mkoa wa Mara nchini Tanzania. Mradi pendekezwa unamilikiwa na Mgodi wa Dhahabu wa North Mara (NMGM) ambayo ni kampuni ya utafutaji na uchimbaji madini inayomilikiwa na kampuni ya Twiga Corporation, iliyoundwa kwa ubia kati ya Barrick (84%) na Serikali ya Tanzania kwa (16%). Eneo la Mradi liko chini ya Leseni ya Uchimbaji Maalum (SML 17/96). Mradi pendekezwa unazigusa kata nne ambazo ni Nyamwaga, Nyarokoba, Kibasuka na Kemambo pamoja na sehemu za vijiji vitano: Komarera, Genkuru, Msege, Kewanja na Nyakunguru.

Upanuzi wa mashimo ya Gena na Gokona ni muendelezo wa shughuli za uchimbaji pamoja na faida za kiuchumi zitokanazo na shughuli hizo za uchimbaji. Kwa miaka mingi, NMGM imekua ikiendeleza tafiti katika eneo hilo ambazo zimeonyesha uwepo wa mashapo yaliyopo kwenye mashimo hayo.

Ili kutekeleza Mradi pendekezwa, Tathmini ya Athari za Mazingira (TAM) itafanyika kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, Kanuni za Tathmini ya Athari za Mazingira ya mwaka 2005 na marekebisho yake ya mwaka 2018 pamoja na Sheria ya Madini ya mwaka 2010.

NMGM imeziteua kampuni za Digby Wells Environmental na PAULSAM Geo-Engineering Limited kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM). Utafiti huo utachunguza athari chanya na hasi kwenye mazingira na jamii zitakazotumika kuunda Mpango wa Usimamizi wa Mazingira kwenye utekelezaji wa Mradi.

Kwa kuzingatia utaratibu, usajili pamoja na uwasilishwaji wa taarifa za awali za mradi kwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) unaendelea kama sehemu ya TAM. Tangazo hili linawakaribisha watu wote wenye nia, ushauri au maarifa kuhusu athari zozote ama za kimazingira au kijamii zinazohusiana na mradi huu kuwasilisha mawazo yao kwa kupitia anuani zifuatazo:

| Mdhibiti | Muwekezaji | Wataalamu washauri elekezi |
|---|---|---|
| Mkurugenzi Mkuu<br>Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (NEMC),<br>S.L.P. 63154, Regent Estate,<br>Dar es Salaam, Tanzania.<br>Simu: +255 22 2774889<br>Barua pepe: dg@nemc.or.tz | Mgodi wa Dhahabu wa North Mara (NMGM)S.L.P. 422<br>Tarime<br>Tanzania<br>Faksi: 255282621903<br>barua pepe: apolinary.lyambiko@barrick.com | PAULSAM Geo-Engineering Company Limited,<br>Ghorofa ya 07 , Faykat Tower Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, Dar es Salaam, Tanzania.<br>S.L.P. 70812<br>Simu/Faksi: +255 755561188<br>Barua pepe: piliseleman@gmail.com |
| | | ESD Advisory Ltd T/A Digby Environmental<br>Madai Crescent, Plot 151, Ada Estate, Dar es Salaam.<br>Jamii:+255717087482<br>Barua pepe: Deogratius.lorri@digbywells.com |

**Ushirikishwaji wa wadau utafanyika kama sehemu ya mchakato wa TAM ambapo habari zaidi zinazohusiana na mradi zitawasilishwa.**

216778302

# Mjamzito apigwa na radi na kufariki dunia

**Na Said Hamdani, LINDI**

MJAMZITO Asumini Andrew (33), mkazi wa Kata ya Kiwalala, Halmashauri ya Mtama, ameuawa kwa kupigwa na radi wakati akitoka shambani.

Tukio hilo lililothibitishwa na uongozi wa kata lilitokea Aprili 4, saa 10:30 alasiri.

Ofisa Mtendaji Kata ya Kiwalala, Zaituni Lichinga alisema, siku hiyo ya tukio, Asumini akiwa ameongozana na mama yake mzazi, Arafa Matingo, alipigwa na radi hiyo iliyoambatana na mvua na kufariki papo hapo.

Alisema kutokana na kishindo cha radi, mama wa marehemu, alidondoka chini na kupoteza fahamu na kukutwa na wapita njia waliokuwa wakirejea nyumbani wakitoka mashambani.

Matingo alimwambia mwandishi wa habari hizi kuwa akiwa ameongozana na mwanawe aliyekuwa na ujauzito wa miezi mitano, mvua iliyoambatana na radi iliwakuta na kuwapiga na kuwadondosha chini.

"Mwanangu alikuwa mbele yangu na mimi nikiwa nyuma, radi ilipopiga sote tulidondoka chini, mwanangu akafariki papo hapo," alisema Arafa.

**Alisema kutokana na kishindo cha radi, mama wa marehemu, alidondoka chini na kupoteza fahamu na kukutwa na wapita njia waliokuwa wakirejea nyumbani wakitoka mashambani.**

# LATRA yaita wadau kujadili nauli mpya

**Na Romana Mallya**

WAKATI Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ikiwaita wadau wa usafiri ili kutoa maoni yao kuhusu mapendekezo ya viwango vya nauli za usafiri, Shirikisho la Viwanda Tanzania (CTI) limeitaka serikali kupunguza ushuru na tozo katika mafuta ili kuweka sawa bei.

Kwa mujibu wa tangazo la LATRA jana kupitia Mkurugenzi Mkuu wake, mkutano huo wa kupokea maoni utafanyika Aprili 13, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

"Maoni hayo yatapokelewa kwa utaratibu wa aina mbili za huduma, kwa mabasi ya safari ndefu na mabasi ya usafiri wa mijini," ilisema taarifa hiyo.

Naye, Ofisa Sera za Biashara kutoka Shirikisho la Viwanda Tanzania (CTI), Frank Dafa, alisema mafuta ni bidhaa ambayo hutumika katika viwanda vyote vya uzalishaji.

Alisema hili ni tukio la kidunia ambalo Tanzania haiwezi kujitenga hivyo inahitaji sera madhubuti kwa kuwashirikisha wazalishaji.

"Kwa mfano wazalishaji wa bidhaa za ngano wanaomba kupunguziwa ushuru wa forodha kutoka asilimia 10 kuwa asilimia sifuri kwa mwaka mmoja katika mapendekezo ya bajeti ya mwaka 2022/23 ili kuwawezesha kuzalisha kwa ushindani na kudhibiti kupanda kwa bei zao," alisema.

Dafa alisema viwanda vitaathirika moja kwa moja na kutolea mfano wazalishaji wa bidhaa za majumbani wanatakiwa kuzisafirisha kwenda kwenye masoko na maeneo mengineyo.

"Serikali kupitia bajeti ya mwaka 2022/2023 wanapaswa kupunguza ushuru na tozo katika mafuta ili kuweka sawa bei ya mafuta.

"Inapaswa pia kujifunza kutoka nchi za Afrika Mashariki ambao wamechukua hatua ya kuimarisha kwa kuweka mifuko maalum ili kuweza kuimarisha bei ya mafuta kuwa linganifu."




Barabara ya kwenda sokoni Buguruni, jijini Dar es Salaam jana, ikiwa imefurika maji machafu na kusababisha kero kwa wananchi wanaotumia barabara hiyo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ajitosa baharini na kufa akiwakimbia polisi

**Na Said Hamdani, LINDI**

MKAZI wa mtaa wa Sabasaba, Kata ya Jamhuri, Manispaa ya Lindi, Hassani Mussa M'buyu (27), amekufa maji, baada ya kujitosa baharini kwa madai ya kukimbia kukamatwa kwa tuhuma za kutishia kumuua mpenzi wake.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, ACP Mtatiro Kitinkwi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

Alisema M'buyu ambaye ni mwendesha bodaboda, alichukua uamuzi huo, Aprili 4, mwaka huu, saa 12:30 jioni.

Kamanda Kitinkwi alisema, M'buyu alifikishwa Kituo cha Polisi Lindi mjini kwa tuhuma za kumpiga na kumtishia kumuua mpenzi wake Sharifa Zakaria Mussa (23).

Alisema baada ya mlalamikaji kuwasilisha madai hayo, askari kupitia dawati la jinsia lilichukua jukumu la kumuandikia M'buyu barua kumtaka kufika kituoni kwa mahojiano kuhusu madai yaliyowasilishwa na mpenzi wake.

"Huyu M'buyu baada ya kufika kituoni pale, alielekezwa aende chumba cha dawati la jinsia," alisema Kamanda.

Kamanda alisema baada ya mlalamikiwa kufika mlango wa chumba cha dawati, alimkuta mpenzi wake akiwa ndani ameshawasili na kuamua kuchukua hatua ya kukimbia, askari walivyomuona walimkimbiza, lakini alikataa kusimama na kujitosa baharini na kufariki.

"Kituo chetu cha polisi hapa Lindi mjini kipo kama umbali wa mita 100 kufika baharini," alisema Kitinkwi.

Sharifa akizungumza na mwandishi wa habari hizi, alisema yeye na M'buyu walikuwa wapenzi na kubahatika kubeba ujauzito, lakini hakuwa anampatia huduma yoyote.

Alisema hata alipolazwa hospitalini akisumbuliwa na maumivu ya tumbo hakuwahi kwenda kumuona kumjulia hali, huku gharama zote za matibabu zikitekelezwa na mama yake mzazi, hatua iliyomlazimu kukatisha mahusiano yao.

Sharifa alisema uamuzi huo ulimjengea uhasama na mpenzi wake kwa kumpa kichapo na kumtishia kumuua iwapo ataendelea na uamuzi wake wa kumkataa kwa kumkata mapanga, hali iliyomlazimu kwenda kituo cha polisi kutoa taarifa ya usalama wa maisha yake.


**TANGAZO**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**

# TANROADS

## KUMBUKIZI YA KIFO CHA SHEIKH ABEID AMANI KARUME



Mtendaji Mkuu, Menejimenti na Wafanyakazi wa **TANROADS** tunaungana na **Mhe. Dkt. Hussein Ally Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kumbukizi ya **miaka 50** ya Kifo cha **Sheikh Abeid Amani Karume,** Rais wa Kwanza wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

**TANROADS** tutaendelea kukuenzi daima.

**TANROADS** Makao Makuu
Ghorofa ya 3, 10 Barabara ya Shaaban Robert / Garden Avenue
S.L.P 11364 Dar Es Salaam Baruapepe:Tanroadshq@tanroads.go.tz

***www.tanroads.go.tz***

***MIUNDOMBINU BORA YA BARABARA, VIWANJA VYA NDEGE NA MADARAJA KWA MAENDELEO YA TAIFA***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali sasa ifuatilie kwa karibu upandaji holela bei za bidhaa

**JUZI** Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) ilitangaza bei mpya za mafuta ikiwa na ongezeko la Sh. 321 kwa lita ya petroli , Sh. 289 kwa dizeli na Sh. 474 ya taa yanayopokelewa Bandari ya Dar es Salaam.

Aidha, kwa Bandari ya Tanga ongezeko ni Sh. 85 kwa petroli na Sh. 295 kwa dizeli, huku wanaochukulia Bandari ya Mtwara ni ongezeko la Sh. 281 kwa dizeli huku petroli ikibaki kwa bei ya zamani.

Kupanda kwa mafuta moja kwa moja kunakwenda kuongeza bei ya bidhaa mbalimbali na kuongeza ugumu wa maisha.

Jana Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwasilisha makadirio na mapato ya ofisi yake kwa mwaka wa fedha 2022/23, aliagiza wazalishaji na wasambazaji wa bidhaa muhimu kushusha bei walizopandisha pasipo kuendana na uhalisia wa soko.

Alisema hivi karibuni kumekuwapo taarifa za uhaba na upandaji wa bei usioendana na uhalisia wa soko katika bidhaa za ujenzi, vyakula, nishati na pembejeo za kilimo.

Kimsingi, tangu Rais Samia Suluhu Hassan, alipoeleza umma kuwa kupanda kwa bei ya vitu hakutaepukika kutokana na athari ya vita ya Russia na Ukraine, baadhi ya wafanyabiashara walipandisha bidhaa zao.

Aidha, wengine walipandisha kwa kisingizio cha UVIKO-19, licha ya serikali kutoa onyo mara kadhaa ikiwamo kufanya tathmini ya bei ya bidhaa hizo, lakini bado zilizidi kupanda.

Mathalani, vifaa vya ujenzi vilizidi kupanda bei kabla ya vita, mfano nondo ya milimita 12 ilitoka Sh. 19,500 hadi 26,000, misumari kutoka Sh. 3,000 hadi 3,500, huku sababu kubwa ikiwa ni kupanda kwa bei ya chuma.

Pia, mafuta ya kula ya alizeti yalianza kuadimika na baadaye kupanda bei kutoka Sh. 4,500 lita moja hadi sasa ni Sh. 10,000, huku sabuni ya mche ikipanda kutoka Sh. 2,500 hadi 3,500.

Bidhaa nyingine ni gesi ambayo ilipanda toka Sh. 45,000 mtungi wa kg 30 hadi Sh. 55,000, hali iliyowalazimu wananchi wengi kurudi kwenye kutumia mkaa, au kupandisha bei ya vitafunwa na chips.

Kwa sasa rasmi EWURA imetangaza bei mpya ambazo zimepanda kwa kiasi kikubwa katika historia ya Tanzania, maana yake hakuna namna ya kuzuia kupaa kwa bidhaa hizo.

Kwa ujumla kauli za serikali kuwataka wafanyabiashara kushusha bei za bidhaa mara kadhaa, lakini imekuwa ngumu kutekelezwa kutokana na ukweli kuwa ni soko huria na kwamba wauzaji watashindana kwa kadri ya hali ya soko.

Februari mwaka huu, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, ilifanya tathmini ya hali bei ya bidhaa na kuelekeza wafanyabiashara kutopandisha bei huku ikiahadi kuchukua hatua kali.

Tunatambua wizarani kuna kitengo cha Biashara, ambacho hufuatilia bei za bidhaa kila siku kwenye mikoa mbalimbali na kutoa taarifa, lakini bado haijasaidia kupunguza bei.

Tanzania kuna wasomi wengi wa uchumi wanaoweza kushauri nini kifanyike kuwapunguzia wananchi makali ya maisha, bila kulazimisha wafanyabiashara ambao wanawajibu wa kulipa kodi kupunguza makali.

Kwa nchi zilizoendelea serikali huweka ruzuku kwenye bidhaa, ili kuwasaidia wananchi wasiumie na wauzaji wasipate hasara, lakini kwa nchi zetu ni ngumu zaidi ya kufuatilia kwa karibu hali ya soko ili kuona kama bei siyo ya maumivu.


Ni lazima serikali ifuatilie kwa karibu hali kwenye masoko na maduka, ili kuona bei zinaendana na uhalisia, kwa kuwa wakiachwa kuna uwezekano wa wafanyabishara kujipanga kuwa na msimamo wa bei ambao unawatengenezea faida kubwa, huku ikiamsha umuhimu wa kuwa na umoja wa walaji ili kutetea maslahi ya wengi.

Tunashauri hivyo kwa kuwa uzoefu unaonyesha kuwa katika nchi zinazoendelea hakujawa na uelewa kuhusu mfumo wa soko huru, hivyo tusishangae hata muuza mhogo shambani kwake akipandisha bei kwa kisingizio cha mafuta na makali ya UVIKO-19.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Serikali izitupie jicho taasisi za mazingira zinazojituma vyema

Na Jenifer Gilla

**HIVI** karibuni Jopo la Kimataifa la kupambana na Mabadiliko ya Tabianchi (IPCC), limetoa ripoti mpya ambayo kwa mara nyingine tena, inasisitiza dharura ya kupunguza haraka na kwa kina gesi joto (GHG), ili dunia iepuke athari mbaya zaidi za hali ya hewa.

Ripoti imegundua kuwa uzalishaji wa gesi joto duniani uliongezeka katika muongo mmoja uliopita kwa zaidi ya asilimia 12, ukilinganishwa na mwaka 2010, hali inayorudisha nyuma kasi ya kupunguza ongezeko la joto duniani hadi nyuzi joto1.5.

Ikiwa dunia imebakisha miaka mitatu tu kufikia malengo ya kuzuia ongezeko la joto kufikia nyuzi joto 1.5, ripoti hiyo imeeleza lengo hilo pamoja na kufikia hewa chafu sifuri, halitofanikiwa bila ya kutumia mbinu mbalimbali, kama vile kupanda na kuzuia ukataji miti.

Hapo juhudi za umma zinahamia, kwenye matumizi ya nishati na teknolojia. Ni dhahiri kuwa serikali ya nchi yoyote haiwezi kufikia makubaliano hayo peke yake, bali inahitaji msaada kutoka sekta binafsi na wadau wengine wa mazingira.

Ndio maana serikali ya Tanzania kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, ilipofanya maboresho ya Sera ya Mazingira, ikaja na mpya ya mwaka 2021, kuleta inayoendana na hali ya sasa ya ukuaji teknolojia, kasi ya athari za mabadiliko ya tabianchi na ushirikiano na sekta binafsi.

Lakini, kuonyesha ushirikiano na sekta binafsi katika sera hakutozaa matunda, kama serikali haitoonyesha kwa vitendo kufanya kazi bega kwa bega na watu hawa katika utunzaji mazingira.

> **Shime kwa serikali kuzitafuta na kusaidia kwa hali na mali, kwa kuwa ndio waliopo karibu na jamii, hivyo kazi wanazofanya zina matokeo makubwa kwa kuwa zinafika ambako yenyewe haiwezi kufika**

Tuna taasisi za mazingira zinazofanya kazi nzuri ya utekelezaji wa agizo la asasi kimataifa katika mazingira UNFCC la kuhakikisha kila nchi kwa nafasi yake inapambana na athari za mabadiliko ya tabianchi, ili kufikiwe lengo la mwaka 2025 la kuzuia ongezeko la joto.

Kuna taasisi zinafanya kampeni ya kuhamasisha upandaji wa miti shuleni kwa kuwapa wanafunzi wa shule ya msingi na sekondari elimu ya utunzaji miti, pamoja na kugawa miti inayopandwa katika maeneo hayo.

Pia, kuna zinazomilikiwa na wanawake, ambazo nazo zinafanya kazi nzuri ya kuelimisha jamii hasa vijana na wanawake juu ya athari za mabadiliko ya tabianchi, pamoja na kuwapa njia mbadala kuepuka kukata miti wanawake, ikiwamo kutengeneza mkaa unaotokana na taka.

Hizo pamoja na nyingine nyingi, zinajitoa kuhakikisha Tanzania inafikia malengo ya kupunguza makali ya ongezeko la joto, lakini zinahitaji serikali kuzishika mkono ili ziweze kutimiza malengo hayo.

Shime kwa serikali kuzitafuta na kusaidia kwa hali na mali, kwa kuwa ndio waliopo karibu na jamii, hivyo kazi wanazofanya zina matokeo makubwa kwa kuwa zinafika ambako yenyewe haiwezi kufika.

Si serikali tu, hata mashirika makubwa kama vile 'UN-Enviroment', zinapaswa kuzifikia taasisi ndogo kwa kuzipa msaada kidogo, ikiwemo nauli na vitendea kazi, pia motisha ya kuendelea kufanya vitu vizuri katika muktadha wa kimazingira.

## Serikali yaombwa mfumo kusaidia ukuaji elimu

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI imeombwa kuweka mfumo wa ushirikishwaji wa mawazo ya walimu kuanzia ngazi ya chini ili kusaidia ukuaji wa elimu nchini.

Mkuu wa Kitengo cha Biashara na Masoko cha Benki ya Biashara ya Mwalimu, Leticia Ndongole, alisema hayo wakati wa hafla fupi ya kuzindua huduma mpya ya Ada Chap Chap, ambayo ni mkopo unaosaidia ulipaji wa ada kwa wakati kwa wale wenye changamoto ya kulipa.

Leticia alisema kuja kwa huduma hiyo kumetokana na maoni ya walimu ambao ni asilimia 90 ya wateja wao.

Alisema katika kukusanya maoni ya wateja wao kuhusu huduma zao wamegundua ada ni tatizo kwa wanafunzi na wazazi wao, pia walimu wamebainisha mahitaji ya kuboreshwa miundombinu ya ufundishiaji.

"Kama benki pamoja na changamoto nyingi ambazo walimu wameziainisha, tumeona tusaidie kwenye suala la ada, benki itatoa mikopo kupitia shule na vyuo na mikopo itaanzia kwenye shule za msingi mpaka vyuo mbalimbali ambavyo wazazi wanasomesha kwa kulipia," alisema Leticia.

Aidha, alisema serikali ikiweka mfumo mzuri wa kukusanya maoni ya walimu kutoka chini na kushirikiana na taasisi nyingi inaweza kusaidia kukuza elimu yetu kama taifa.

"Mikopo yetu inalenga kusaidia wanafunzi na wazazi wao, kama mzazi ni mfanyakazi au mjasiriamali basi anaweza kupata mkopo huo kupitia shule au chuo chake na italipwa ndani ya mwaka mmoja," alisema Leticia.

Kwa upande wa shule na taasisi zilizoingia mkataba na benki hiyo kutoa mikopo wamefurahia huduma hiyo ambayo itawasaidia wazazi kutokuwa na mawazo ya kupata ada kwa wakati.

"Huduma hii kwa kweli itatusaidia sisi kama chuo, lakini zaidi itawasaidia walimu na wazazi wao, sisi tumeingia mkataba na mkombozi benki kupokea huduma hii ambapo ada italipwa moja kwa moja kwenye akaunti ya chuo," alisema CPA Godson Mkalo.

Aidha, Injinia Edwin Godwin kutoka taasisi ya kutoa elimu ya uendeshaji mitambo mikubwa (IHET), alisema taasisi nyingine za kifedha ziige mfano wa Mkombozi benki kusaidia kwenye sekta ya elimu.

Baadhi ya shule na vyuo ambazo tayari zipo kwenye mkataba na benki ya Mwalimu ni Eagle High School- Bagamoyo, City College of Health and Allied Sciences kampasi ya Ilala, Goba (Mount Ukombozi) na Covenant Institute of Accountancy and Technology.

Nyingine ni Covenant Financial Consultants kwa wanataaluma wa uhasibu yaani CPA na Institute Heavy Equipment and Technology - Kijitonyama.

## Mbunge ataka wanataaluma vyuoni kutoteuliwa serikalini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Kibamba (CCM), Issa Mtemvu, ameshauri serikali kuacha kuteua wanataaluma wabobezi kwenye vyuo vikuu kujaza nafasi mbalimbali kwa kuwa inasababisha kuwapo na upungufu wao. Mtemvu alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akiuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema kuna utafiti uliofanywa na Chama cha Wafanyakazi wa Elimu ya Juu (THTU) mwaka 2017 ulionyesha kuna upungufu mkubwa wa wanataaluma wakiwamo wahadhiri na maprofesa.

Alisema sababu kubwa iliyotolewa na THTU kuwa ni serikali kutumia wataalamu hao katika kujaza nafasi mbalimbali serikalini.

"Je, serikali haioni sasa ni wakati wa kushauri mamlaka za uteuzi kuacha kutumia wataalamu hasa wahadhiri wabobezi katika nafasi mbalimbali serikalini,"alihoji.

Akijibu, Naibu Waziri wa Elimu, Omary Kipanga alisema: "Kwa kuwa Mbunge ametoa wazo na mamlaka za uteuzi zipo naomba Mheshimiwa Mbunge tuchukue hoja yake hii ili kufikisha kwenye vyombo vya uteuzi ili wafanye tathmini toshelevu iwapo kama wanaona inafaa kufanya hivyo lifanyiwe kazi."

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum(CCM), Dk.Paulina Nahato, alihoji Serikali itatoa vibali kwa vyuo vikuu vyenye upungufu wa wanataaluma wapya.

Akijibu, Kipanga alisema Serikali inatambua tatizo la upungufu wa wanataaluma katika vyuo vikuu vya umma.

"Serikali imekua ikitoa vibali vya ajira kila mwaka ambapo katika mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2020/21, Serikali ilitoa vibali vya nafasi za ajira mpya za Wakufunzi na Wahadhiri Wasaidizi 333 katika vyuo vikuu vya umma,"alisema.

Alisema ili kukabiliana na tatizo hilo Wizara hiyo inaendelea na jitihada za kuomba vibali vya ajira za Wahadhiri kutoka Wizara yenye dhamana na utumishi wa umma na utawala bora.




Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dunstan Kyobya (kushoto), akipokea viti na meza kutoka kwa Meneja Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), Editha Mwakatobe, kwa ajili ya matumizi kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Tangazo, Manispaa ya Mtwara juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Matukio 27,838 ya ukatili yaripotiwa polisi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa matukio 27,838 ya vitendo vya ukatili nchini yameripotiwa kwenye vituo vya polisi ndani ya miaka minne.

Katika matukio hayo vitendo vya ubakaji vimekithiri kwa matukio 19,726.

Hali hiyo, imewafanya wabunge wahoji mkakati wa serikali wa kukabiliana na matukio hayo nchini ili kuondokana na idadi kubwa ya vitendo hivyo.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni alitoa takwimu hizo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti maalum (CCM), Fatma Toufiq, aliyetaka kujua kuna waathirika wangapi wa vitendo vya ukatili nchini kuanzia mwaka 2019 hadi 2022.

Akijibu swali hilo, Waziri Masauni alisema kuanzia mwaka 2019 hadi Machi, 2022 matukio 27,838 yameripotiwa ya ubakaji ni 19,726, kulawiti 3,260 kati yao wanaume 3,077 na wanawake 183.

Pia, matukio ya kuunguzwa kwa moto ni 198 kati yao wanaume 73 na wanawake 125, kutupa watoto wachanga ni 443 kati yao wanaume 177 na wanawake 266, kipigo ni 4,211 kati yao wanaume 16 na wanawake ni 4195.

"Jumla ya kesi zilizofikishwa mahakamani ni 21,063 na watuhumiwa waliohukumiwa ni 14,278 na mashauri mengine yako kwenye hatua mbalimbali za upelelezi na mahakamani," alisema.

Alisema serikali inaendelea kuiasa jamii kutumia vyema taasisi za familia, kaya, jumuiya za kidini na ngazi za vitongoji, vijiji na mitaa kudhibiti vitendo vya ukatili.

Katika swali la nyongeza la Mbunge huyo alisema idadi kubwa ya wanaofanyiwa ukatili ni wanawake na watoto na kuhoji serikali ina mkakati gani wa kuzuia idadi kubwa ili kupunguza ukatili huo.

"Je, serikali ina mkakati gani wa kuwalinda watoto wa kiume ili wasifanyie ukatili," alihoji. Akijibu swali hilo, Masauni alisema suala la kuwalinda watoto sio la serikali pekee na itaendelea kuchukua hatua kali kwa wale wote wanaowafanyia ukatili watoto.

Kadhalika, Mbunge wa Viti Maalum, Tunza Malapo alisema vitendo vya ukatili wa kijinsia vimekuwa vikiongezeka na adhabu mbalimbali zinatolewa, lakini bado vitendo hivyo vinashamiri.

"Je, serikali haioni ni wakati muafaka wa kupitia adhabu hizi ili ziwe kali zaidi na watu wasiendelee kufanya vitendo hivyo vya ukatili," alihoji.

Masauni akijibu swali hilo, alisema serikali itafanyia kazi hoja hiyo.

Naye, Mbunge wa Viti maalum, Sophia Mwakagenda, alisema kumekuwapo na mauaji na vipigo vingi kwasababu za wivu wa mapenzi na kutaka kujua serikali inachukua hatua gani ya kuhakikisha wale wanaofanya vitendo hivyo wanachukuliwa hatua kali ili kukomesha vitendo hivyo.

Akijibu swali hilo, Waziri Masauni alisema kwa kipindi cha Januari hadi Machi, mwaka huu, kumekuwa na mauaji mengi kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo wivu wa mapenzi, ushirikina, ulevi uliokithiri, kugombea mali.

"Tulichukua hatua ya kuunda Tume imefanya kazi vizuri na kupitia mapendekezo mengi katika mambo makubwa, lakini jukumu kubwa na la msingi ni kuhakikisha matukio haya hayajitokezi," alisema.

Alisema miongoni mwa mambo yaliyopendekezwa na tume ni kuimarisha mifumo katika ngazi za kata na hivi karibuni polisi zaidi ya 4,200 walihitimu mafunzo na wamepelekwa kwenye kata ili kuimarisha usalama kwenye maeneo hayo na kudhibiti matukio hayo.

# Ridhiwani awaonya wenyeviti ardhi rushwa

**Na Munir Shemweta,**
TANGA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, amewataka wenyeviti wa mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya nchini kujiepusha na vitendo vya rushwa ili kutenda haki katika kutoa uamuzi katika mashauri yanayohusu ardhi.

Pia amezitaka mamlaka za nidhamu kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wasiotimiza wajibu wao au wanaoidhalilisha serikali kwa kuendesha vitendo vya rushwa.

Wenyeviti wa mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya pamoja na wasajili wasaidizi wanakutana mkoani Tanga kwenye kikao kazi na mafunzo cha siku nne kujadiliana namna ya kuboresha utendaji kazi na utoaji huduma bora kwa wananchi kuhusiana na mashauri ya ardhi.

'Daima tukumbuke ili mabaraza ya ardhi yaheshimike ni wajibu wenu wenyeviti wa mabaraza kama watumishi wa umma kufanya kilicho sahihi yaani kuzingatia weledi, kuwa waadilifu na kuwajibika. Tukumbuke kuwa sisi ni watumishi wa umma ni waajiriwa wa wananchi,'' alisema juzi kwenye kikao kazi hicho.

Naibu Waziri alisema mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya kama vyombo vya kutoa haki, yana wajibu wa kutoa huduma bora kwa wananchi ili kuondoa malalamiko dhidi ya ukiukwaji wa maadili katika kushughulikia migogoro ya ardhi.

''Haki na wajibu ni sawa na chanda na pete katika uwajibikaji wa daraja la juu. Mtekelezaji wa utoaji au usimamizi wa haki bila kuwa mwadilifu ni mtihani mkubwa,'' alisema Ridhiwani.

Kwa mujibu wa Ridhiwani, maadili ni kitu muhimu cha kuzingatia katika utendaji kazi hasa kipindi hiki ambacho serikali inafanya juhudi mbalimbali kuhakikisha watumishi wa umma wanazingatia maadili yanayosimamia utumishi wa umma.

''Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan katika matamshi yake mbalimbali, ameonyesha wazi nia yake ya kuurejesha utumishi wa umma kuwa utumishi uliotukuka na unaozingatia taratibu za utendaji na maadili yanayoongoza utumishi wa umma'' alisema Ridhiwani.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Allan Kijazi, alisema wizara itaanza kuweka mfumo wa ufuatiliaji utendaji kazi wa wenyeviti wa mabaraza ya ardhi kwa lengo la kuboresha utendaji kazi.

''Katika mfumo huo wa ufuatiliaji wale wenyeviti ambao utendaji wao utaridhisha tutakuwa pamoja na wale wasiotaka kubadilika itabidi watupishe na tutafute watendaji au wenyeviti walio tayari kutekeleza majukumu na wako tayari kutenda haki kwa watanzania wote bila kubagua. Kikubwa zaidi kuwa tayari kubadilisha taswira ya wizara ya kiutendaji kutoka wizara ya malalamiko na kuwa wizara yenye kupewa sifa nzuri za utendaji,'' alisema.

Naye Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, Stella Tullo, alisema mafunzo waliyoyapata wenyeviti wa mabaraza ya ardhi yatawajengea uwezo na anaamini watakaporudi kwenye vituo vyao vya kazi, watakuwa na nafasi nzuri ya kusikiliza mashauri ya ardhi sambamba na kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora.



Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo (katikati), akikata utepe kuzindua rasmi Tawi la Benki ya Biashara Tanzania (TCB) Mbagala Chalambe, mkoani Dar es Salaam jana. Wengine ni Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Moses Manyatta (kushoto) na Meneja wa Tawi hilo, Edward Mwoleka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## 'Msiwakate watoto kimeo wanaweza kupata Ukimwi'

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Kitengo cha Watoto Mahututi Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Yasser Said, amewataka wazazi kuacha kuwakata watoto wao kimeo kwa sababu yapo madhara yanayoweza kumsababishia mtoto kifo au kupata maambukizi ukiwamo UKIMWI.

Dk. Said alisema jana kuwa katika jamii imekuwa ni kawaida kwa wazazi au walezi kuwakata watoto wao kimeo ambacho ni kinyama kidogo kinachokaa kwenye kinywa upande wa juu.

"Kimeo kina kazi kuu ya kuzuia chakula kisipande eneo la pua la juu ili usipaliwe, mtu anayekata kimeo ataendelea kupaliwa tu tofauti na wale ambao hawajakatwa," alisema.

Alisema madhara ambayo hujitokeza ni kuvuja damu kwa wingi hadi kumsababishia umauti.

"Ipo nafasi kubwa kupata maambukizi ya homa ya ini, UKIMWI na tetenasi, jamii ifahamu panapotokea tatizo la kukohoa kituo cha kwanza ni kupata ushauri wa daktari," alishauri.

Dk. Said alitaja sababu kubwa ya watu kukata kimeo huwa ni baada ya kumwona mtoto anakohoa.

"Watoto wengi wanapokohoa wazazi wanashauriana inawezekana ni kimeo, zipo sababu nyingi zinazosababisha mtu kukohoa inawezekana ikawa pumu, nimonia au kifua cha kawaida, ninaomba jamii ifahamu mtoto anapokohoa msikimbilie kukata kimeo wafuate ushauri wa daktari," alishauri.

Alitaja madhara ambayo hujitokeza mtu anapokatwa kimeo na tangu mwaka huu uanze amepokea watoto watatu wote wakiwa wameshakatwa na wawili wamefariki.

Maua Juma, mkazi Kiwalani Minazi Mirefu, alisema yeye ni mhanga wa mtoto aliyekatwa kimeo baada ya kumwona anatapika na kukohoa alishauriwa na watu wa karibu akakatwe.

Alisema baada ya kukatwa mtoto akapata matatizo makubwa ikiwamo kutapika damu, kunya choo cheusi na hali yake ikawa mbaya.

"Nilikwenda hospitali ya jirani wakashindwa nikapewa rufaa nikaja Muhimbili walivyonipokea hali ilikuwa mbaya madaktari wamepigana mpaka hapa sasa anaendelea vuzuri. Ushauri wangu kwa jamii siyo kila kifua au kutapika ni kimeo," alishauri.

## TCB yatumia mwaka mmoja kukopesha bil. 7.2 Mbagala

**Na Mwandishi Wetu**

Tawi la Mbagala la Benki ya Biashara Tanzania (TCB) limekuwa na mwaka mmoja wa mafanikio makubwa kiutendaji na kusaidia kufanikisha azma ya taasisi hiyo ya kupeleka huduma jumuishi za kifedha kwa watu wengi.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi rasmi wa tawi hilo lililopo Rangi Tatu, Chalambe mkoani Dar es Salaam, Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Mosese Manyatta, alisema moja ya mambo makubwa yaliyofanywa na tawi hilo ni kutoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 7.2. aAlimweleza mgeni rasmi wa shughuli hiyo, Mkuu wa

Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, kuwa uwekezaji katika tawi hilo umewanufaisha maelfu ya wakazi wa Mbagala wakiwemo wateja 564 waliokopa.

"Tangu kufunguliwa kwake Januari mwaka jana, Tawi la TCB Mbagala limepata mafanikio makubwa na kukua kwa kasi ikiwamo kufanikiwa kukusanya amana za wateja zenye thamani ya Sh. bilioni 4," alibainisha Manyatta.

Jambo jingine kubwa ni umahiri wa wakazi wa Mbagala kurejesha mikopo," alisema na kuongeza kuwa jambo hilo kwa sasa linafanyika kwa zaidi ya asimilia 99. Kwa mujibu wa Manyatta, hii imepelekea tawi hilo kuwa na uwiano ndogo wa mikopo chechefu miongoni mwa matawi ya benki hiyo wa asilimia 0.8.

Aidha, alimwambia DC Jokate kuwa tawi hilo jpya linafanya idadi ya matawi ya TCB mkoani Dar es Salaam kufikia 20 huku manane yakiwa katika Wilaya ya Temeke.

Uwekezaji wa Mbagala unaifanya taasisi hiyo kongwe ya fedha kuliko zote nchini kuwa na jumla ya matawi 85 na kuifanya kuwa miongoni mwa benki shindani sokoni.

Matawi haya yanasaidiwa na mawakala zaidi ya 3,000 kuwahudumia wananchi na

kuzipeleka huduma za benki hiyo na karibu walipo. Pia TCB ina wigo mpana wa ATMs zaidi ya 80 inazozimiliki na nyingine 300 zilizo kwenye mfumo wa Umoja Switch unaojumuisha benki 20.

DC Jokate aliipongeza TCB kwa kuwa kinara wa huduma jumuishi za kifedha na kusema uwekezaji inaoufanya kuwahudumia wananchi unaenda sambamba na juhudi za serikali za maisha bora kwa wote.

Katika kulifaniksha hilo, alifafanua, serikali inashirikiana kwa karibu na wadau kamaTCB kuhakikisha kuwa Watanzania wanapata huduma bora na nafuu za kibenki pamoja na suluhisho bunifu kama akaunti maalum ya wanawake ya GTCVB Tabasamu.

Alisema ana matumaini makubwa kuwa uzinduzi wa Tawi la TCB la Mbagala utaendeleza kuchochea maendeleo ya eneo hilo na kuwakwamua kiuchumi wakazi wa Mbagala.

"Sisi kama Serikali tutahakikisha tunaisaidia TCB kuwahudumia wananchi wa Mbagala lakini na nyie hakikisheni huduma zenu zinapatikana kwa urahisi na mnaelimisha watu kuhusu masuala ya fedha.

## Watakiwa kutoficha watoto kwenye sensa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZAZI na walezi mkoani Shinyanga, wanaoishi na watoto wenye ulemavu, wameonywa kutowaficha watoto hao wakati wa sensa ya watu na makazi itakayofanyika Agosti mwaka huu.

Sensa ya watu na makazi inatarajiwa kuanza nchini kote Agosti mwaka huu.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya watu wenye ulemavu mkoani Shinyanga, Richard Mpongo, alitoa rai hiyo wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema sensa ni muhimu sana, na kuwasihi wazazi na walezi wenye watoto ambao wana ulemavu wasije wakajaribu kuwaficha watoto hao, bali wawape fursa ya kuhesabiwa, ili serikali ipate pia idadi kamili ya watu wenye ulemavu na kuwa rahisi kuwasaidia.

"Naipongeza serikali kwa maandalizi ya sensa ya watu na makazi, ni muhimu sana katika upangaji wa mipango ya maendeleo kwa wananchi wake, sababu itakuwa na idadi ya watu kamili kwa kila mkoa,"alisema Mpongo.

"Niwasihi wazazi na walezi ambao wanaishi na watoto wenye ulemavu, wasiwafiche bali nao wahesabiwe, ili serikali ipate na idadi kamili ya watu wenye ulemavu, na inapokuwa ikipanga mipango yake na sisi tupate haki zetu kwa usawa."aliongeza.

## Akabidhiwa gari ushindi wa Tesa Kimilionea

**Na Mwandishi Wetu**

Kampuni ya simu ya mkononi ya Airtel Tanzania imekabidhi gari mpya aina IST kwa mshindi wa kwanza kwenye promosheni ya Tesa Kimilionea.

Airtel imekuwa ikitoa fedha taslimu Sh. 100,000 kwa washindi 100 pamoja na Sh. 1,000,000 kwa kila wiki, huku kwenye droo kubwa ambayo inachezwa kila mwisho wa mwezi washindi wawili ushinda Sh. 10,000,000 na mwingine gari mpya aina ya Toyota IST.

Akizungumza wakati wa kukabidhi zawadi ya gari mpya aina ya Toyota IST kwa mshindi huyo ambaye ni Mchite Mchite, mkazi wa Mbangala jijini Dar es Salaam, Meneja Uhusiano Airtel Tanzania, Jackson Mmbando, alimpogeza kwa kuwa mshindi wa kwanza kujishindia zawadi ya gari kwenye promosheni hiyo.

'Hii ni promosheni maalum kwa wateja pamoja na mawakala wa Airtel wanafanya miamala mbalimbali kwa kutumia Airtel Money kuwa mshindi. Nawaomba wateja pamoja na wakala wa Airtel Money kutambua kwamba kila unapofanya muamala wowote kwa kutumia Airtel Money basi unaingia moja kwa moja kwenye droo na hivyo kuwa kwenye ya kujishindia zawadi mbalimbali kama Sh. 100,000, Sh. 1,000,000 kwa droo ya wiki na zawadi kubwa ya Sh. 10,000,000 au gari mpya aina ya IST kwa kila mwezi," alisema.

# Prof. Ngowi alivyofundisha kubadili vikwazo kuwa fursa

**Na Jenifer Gilla**

LEO tunaendelea na somo alilokuwa anatoa aliyekuwa Profesa wa Uchumi wa Chuo Kikuu Mzumbe, marehemu Honest Ngowi, ambaye kupitia Ngowi TV alielimisha wananchi, ambaye alifundisha umuhimu wa kugeuza changamoto kuwa fursa.

Somo hilo alilitoa kwa mfano dhahiri, akiwa katika shamba lake kubwa lililojaa mifugo yenye afya ikiwamo kuku wa nyama na mayai, bata na sungura na mazao yaliyostawi vizuri ikiwamo mapasheni, pembezoni mwa bwawa kubwa lililojaa maji muda wote.

Alisema sababu ya kuanzisha bwawa hilo ni kupunguza gharama ya matumizi ya maji katika biashara hiyo kwa kuwa awali alitumia Sh.90,000 kwa wiki kununua maji boza moja kwa ajili ya shughuli hiyo.

Alisema katika kupitia changamoto ya gharama kubwa za kununua maji ndipo akapata wazo la kutumia fursa ya kuwapo na mkondo mkubwa unaopitisha maji ya mvua eneo lake, hivyo akapata wazo la kujenga bwawa hilo na kuweka njia ya kupitisha maji kutoka kwenye mkondo huo pindi mvua inaponyesha.

"Mvua ikinyesha hayo maji ya kwenye mkondo yalikuwa yakipitia tu na kwenda kupotea kwingine, halafu baada ya siku moja natakiwa nikanunue maji ya Sh.90,000 wakati nimeyaacha hayo yapite, kama mjasiriamali hii ni fursa ambayo ilikuwa inapotea,"alisema Prof. Ngowi.

Alisema kuwa mwanzoni bwawa hilo lilikuwa linahifadhi maji ya kuhudumia mifugo pamoja na mazao kwa miezi sita na baadaye aliliongeza na kufikia kuhudumia kwa mwaka mzima likiwa na lita 3,192,000 , sawa na kunywesha jiji la Arusha kwa siku moja.

Alisema uwepo wa bwawa hilo utamsaidia kufikia malengo ya ndoto zake katika ujasiriamali huo, kwa kuwa umepunguzia gharama kubwa kuliko zote katika uendeshaji wa mradi huo .


Baada ya ufafanuzi huo Prof. Ngowi alisema kuwa mvua zinazonyesha nchini zinatosha kutoa maji nchi nzima na ni fursa kwa wajasiriamali wa mifugo na kilimo kama zikitumiwa ipasavyo.

Alisema ujenzi wa mabwawa ya kuhifadhia maji ni moja ya uwekezaji wa muda mrefu ambao humpunguzia mjasiriamali mzigo mkubwa wa kutafuta maji hasa Dar es Salaam yanapouzwa bei ya juu.

"Katika ujasiriamali wa kilimo na ufugaji hasa katikati ya jiji ndoto kubwa ya mkulima ni upatikanaji wa maji, ukishapata maji unakuwa umerahisisha shughuli hii kwa hivyo wajasiriamali waangalie uwekezaji wa bwawa kama hili," alifafanua.

Akiwa kama mtaalamu wa 'managerial economics' (msimamizi wa uchumi) amekuwa kitumia bwawa hilo kuwafundisha wanafunzi wake namna ya kuona fursa na kuzitekeleza kwa vitendo akiamini njia hiyo humsaidia mwanafunzi kuelewa vizuri tofauti na kutegemea nadharia pekee.

"Mifano kama hii inamsaidia mwanafunzi kuelewa kuwa kumbe hivi tunavyovisoma vinatekelezeka, aah kumbe vinawezekana kufanyika hata Tanzania na siyo Marekani pekee," alisema.




Mkurugenzi wa huduma za Airtel Money, Isack Nchunda (katikati), akikabidhi funguo za gari kwa mshindi wa kwanza wa droo kubwa ya promosheni ya Tesa Kimilionea, Mchita Yusuf Mchita, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waandamana kupinga balozi CCM kuadhibiwa

**Na Julieth Mkreri,** KIBAHA

BAADHI ya wananchi na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mtaa wa Lulanzi Matunda uliopo Kata ya Picha ya Ndege Kibaha wameandamana hadi katika ofisi ya CCM tawi la Lulanzi kupinga adhabu dhidi ya balozi wao, Saimoni Kushoka ya kuzuiwa kufanya siasa kwa kipindi cha miezi 12.

Maandamano hayo yalifanyika juzi katika ofisi hizo saa chache baada ya Balozi Kushoka kukabidhiwa barua maalum kutoka ofisi ya tawi hilo kuhusiana na kufungiwa kutokana na masuala ya siasa katika kipindi hicho.

Mmoja wa wananchi hao, Athumani Said, alisema wameshtushwa na taarifa ya balozi wao kuzuiwa kufanya siasa kwa kipindi kirefu, hivyo kulazimika kuandamana kujua sababu ya adhabu hiyo.

Said alisema kuwa wakazi wa Mtaa wa Lulanzi Matunda wamekuwa wakimtegemea Kushoka katika mambo mbalimbali ya kijamii hasa katika ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo, lakini anashangazwa kuona amepewa adhabu kipindi hiki cha kuelekea katika uchaguzi ndani ya chama.

Aliongeza kuwa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi ndani ya chama walikuwa wakimtegemea Kuchoka achukue fomu kwa ajili ya kugombea nafasi ya ujumbe wa CCM katika tawi hilo, lakini ghafla wakashangaa anapewa barua ya adhabu.

"Huyu Kushoka sisi tunamhitaji sana katika eneo letu kwa ajili ya kusimamia na kufuatilia miradi yetu ya maendeleo, lakini tumeshangaa wakati anakuja kuchukua fomu ya kugombea nafasi ya ujumbe anakutana na barua ya adhabu jambo ambalo hatujaliafiki,"alisema Said.

Nae Martha Kalinga alisema kuwa Kushoka ni mchapakazi ambaye amekuwa ana msaada mkubwa katika Mtaa huo, huku akimuelezea kupigania eneo hilo kupewa hati miliki eneo ambalo awali walitakiwa kuondolewa na Serikali kwa madai ya kuwa wavamizi.

Martha alisema,wanachotaka wao adhabu ya Kushoka iondolewe ili aweze kuchukua fomu kwa kuwa ndiye mtu sahihi wanayemhitaji katika eneo lao, na kwamba hawapo tayari kuchaguliwa mtu wala kuletewa mtu mwingine katika eneo lao.

Kushoka,alisema alipewa barua ya kusimamishwa kujihusisha na siasa katika kipindi cha miezi 12 kutoka kwa mwenyekiti wa tawi la CCM Lulanzi, Michael Ngosi Aprili 1,2022.

Kushoka, alisema siku aliyopewa barua hiyo ni siku ambayo fomu zilikuwa zimeanza kutolewa na kwamba alipofika ofisini hapo alishangaa anapewa barua ya adhabu.

Hata hivyo, Michael Ngosi,alisema ofisi ya tawi haina makosa kwa kuwa barua waliyompa Kushoka imetoka katika ofisi ya CCM Kata ya Picha ya Ndege.

Katibu wa CCM Kata ya Picha ya Ndege, Ally Lwambo, alisema barua ya kusimamishwa Kushoka imetokana na maamuzi ya kamati ya siasa katika kikao chake kilichofanyika Machi 15 mwaka huu na kwamba hatua hiyo ilitokana na balozi huyo kuandika barua ya malalamiko ya kuwatuhuma viongozi akiwamo Diwani wa kata hiyo kupanga safu za uchaguzi huo.

# Waziri Masauni awakana wenye magari ya ving'ora

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, ameliambia Bunge kuwa hajawahi kutoa vibali vya matumizi ya magari ya ving'ora kwa magari ambayo hayajatajwa kwenye Sheria ya Usalama barabarani.

Masauni aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Ukonga (CCM), Jerry Silaa.

Katika swali lake, Silaa alisema kwa Mkoa wa Dar es Salaam magari ya ving'ora ambayo hayastahili yamekuwa ni kero na ni kinyume cha sheria.

"Kupitia kifungu cha 54 cha sheria ya usalama barabarani sura ya 168, je waziri ameshatoa vibali vingapi hadi sasa vya utumiaji wa ving'ora kwa magari mbali na magari yanayotakiwa kisheria," alihoji.

Pia, Mbunge huyo alihoji mpango wa serikali wa kufanya marekebisho ya sheria hiyo ambayo ni ya muda mrefu ili kutoa adhabu stahiki kwa watu wanaovunja sheria hiyo na kuangalia namna ya kuongeza viongozi wanaostahili heshima hiyo ili kuondoa taharuki kwa wananchi.

Akijibu maswali hayo, Waziri Masauni alisema tangu amepewa dhamana ya kuwa waziri hajawahi kutoa kibali chochote cha matumizi ya magari ya ving'ora.

Kuhusu mabadiliko ya sheria, alisema kuna mchakato unaendelea wa mabadiliko ya sheria ya usalama barabarani na kumshauri Mbunge kuandaa hoja zake za kuongeza yanayofaa kwenye marekebisho hayo yatakapofika bungeni.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alihoji sheria gani inasimamia orodha ya wanaostahili kutumia ving'ora na vimulimuli kwa misafara ya viongozi na wananchi wa kawaida.

Akijibu swali hilo, alisema sheria ya usalama barabarani sura ya 168 ya mwaka 1973 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002 ndiyo inayosimamia matumizi ya ving'ora na vimulimuli barabarani.

Kifungu 39 (b)(1)(2) cha sheria kinaelekeza matumizi ya ving'ora na vimulimuli barabarani ambayo ni kutoa ishara kwa watumiaji wengine wa barabara kuchukua tahadhari kuwa kuna dharura.

"Kifungu cha 54 kifungu kidogo cha 1 hadi cha 5 kinaeleza utaratibu na mazingira ya matumizi ya ving'ora na vimulimuli," alisema.

Alitaja magari yanayostahili kutumia ving'ora na vimulimuli kwa mujibu wa sheria ni magari ya Polisi, Zimamoto, magari ya wagonjwa (Ambulance), magari ya vikosi vya ulinzi na usalama pamoja na magari yaliyopata kibali maalumu kutoka kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na kutangazwa katika gazeti la serikali.



Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, akiuliza swali kuhusu utekelezaji wa ahadi ya Waziri Mkuu, aliyoitoa mwaka 2017/2018 ya ujenzi wa kituo cha afya Ulowa, kilichopo jimboni kwake, wakati wa kikao cha Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Mbunge aomba ujenzi kituo cha polisi Nanyamba

SERIKALI imetakiwa kujenga kituo cha polisi Nanyamba mkoani Mtwara kutokana na kilichopo ni kidogo na hakitoshelezi mahitaji ya sasa ikiwamo usalama katika mpaka wa Msumbiji.

Akiuliza swali la nyongeza bungeni jana, Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, alihoji mpango wa serikali kujenga kituo hicho kutokana na kuwapo tatizo la wakimbizi kwenye mpaka na kwa sasa Nanyamba ni Makao Makuu ya Halmashauri ya Mji wa Nanyamba.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yussuf Masauni, akijibu swali hilo, alisema serikali ina mpango wa kujenga vituo, kukarabati na kwamba katika bajeti ijayo serikali imepanga kujenga Makao Makuu ya Polisi Mtwara.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Ukerewe (CCM), Joseph Mkundi, alitaka kujua mkakati wa serikali kukifanyia ukarabati kituo cha Polisi cha Nansio.

Akijibu swali hiyo, Masauni alisema serikali inatambua uchakavu wa kituo cha Polisi Nansio Ukerewe na tathmini kwa ajili ya ukarabati imefanyika mwaka huu, 2022 na kubaini Sh. milioni 68 zinahitajika ili kugharamia ubadilishaji paa, dari, mfumo wa majisafi na majitaka, kuziba nyufa, kurekebisha sakafu na kupaka rangi.

"Ukarabati huu utafanyika kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, naitumia fursa hii kutoa wito kwa wadau wenye nia njema kusaidia uboreshaji wa vituo vya polisi vilivyo kwenye maeneo yao kwa kushirikiana na Wakuu wa polisi wa mikoa na wilaya," alisema.

# Serikali yatakiwa kutoa kauli ushuru bidhaa za ngozi

MBUNGE wa Viti maalum, Halima Mdee ameitaka serikali kutoa kauli kuhusu malalamiko ya wadau wa ngozi kuhusu ushuru mkubwa unaotozwa bandarini na vikwazo vya kusafirisha bidhaa hiyo nje ya nchi.

Akijibu swali hilo bungeni jana, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema viwango vya ushuru wa kusafirisha ngozi ghafi na ngozi iliyosindikwa kiwango cha kati (Wet blue) nje ya nchi ni makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Alisema walikubaliana kuwianisha viwango vya ushuru kwa lengo la kuhakikisha viwanda vya ndani vinapata malighafi ya kutosha kuzalisha bidhaa za ngozi.

"Ushuru wa kusafirisha ngozi ghafi nje ya nchi (export levy) ni asilimia 80 ya thamani ya mzigo ukiwa bandarini (FOB) au Dola za kimarekani 0.52 kwa kilo," alisema.

Alisema ngozi zilizosindikwa kwa kiwango cha kati zinatozwa ushuru wa asilimia 10 ya FOB ili kutoa motisha kwa wasindikaji.

"Ngozi zilizosindikwa hadi kufikia hatua ya mwisho (finished leather) hazitozwi ushuru wowote (0%). Jitihada hizo zimesaidia kuvutia uwekezaji katika viwanda vya kusindika ngozi na kuzalisha bidhaa za ngozi," alisema.

Vile vile, alisema hakuna vikwazo vyovyote katika kusafirisha ngozi, kwa kuwa takwimu zinaonyesha kiwango cha usafirishaji ngozi ghafi kimeendelea kupanda kutoka kilo 513,201 mwaka 2015/16 hadi kufikia kilo 7,370,533 mwaka 2020/21.




Habari zote na Augusta Njoji

ama
ALHAMISI APRILI 7, 2022
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12


**VITA VYA KIFUA KIKUU...**

Hospitali Kibong'oto ilivyoamua kupiga kambi mgodini Mererani



Ukurasa 13

Wataalamu afya: Kunusuru macho ya mtoto mpiganie miaka 4 hadi 9



Ukurasa 14

**Mwenye ulemavu awapa moyo wenziwe kutumia simulizi yake**

AFYA

# Mloganzila yabuni benki akiba maziwa kuwasaidia watoto njiti

**Na Christina Mwakangale**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, imesema katika mikakati yake mwaka huu, ni kuanzisha benki ya maziwa ya mama, lengo ni kuwasaidia watoto njiti ambao kwa asilimia 60 huzaliwa hospitalini hapo.

Dk. Mwanaidi Amir, Bingwa wa Magonjwa ya Watoto na Mkuu wa Idara ya Watoto, Mloganzila, anasema huduma hiyo ni maalumu kwa watoto wenye umri hadi siku 28. Anasema watoto wanaozaliwa njiti, baadhi ya mama zao wanaumwa sana, hivyo anafafanua: "Kinamama ambao wana changamoto ya kupata maziwa tunahofia afya ya mtoto na inaweza kukwamisha ukuaji wao kwa ujumla.

"Tukaona tuanzishe benki ya maziwa. Kuna hatua ambazo zinapitiwa hadi kufanikiwa benki hii kwa sababu mfumo wa uchangiaji ni kama benki ya damu."

Anaeleza, kwanza kunahitajika utayari wa jamii yenye kuunga mkono mpango huo, kwa wananchi walio na maziwa ya kutosha, kulisha mtoto wake kwanza na kisha kumpa mama ambaye hana maziwa.

Pili, ni kuangalia kundi la kinamama wanaoweza kuchangiwa, kwa kuhakisha mchangiaji hana maambukizi ya maradhi kama Ukimwi, homa ya ini na mengine yanayohamishika kwa njia ya damu.

"Tukishapata ridhaa ya wachangiaji, tutaanza kukusanya kwenye benki ambayo itakuwa na uwezo wa kuhifadhi hadi miezi sita," anasema Dk. Mwanaidi.



Mtoto akinyonya. Hospitali ya Mloganzila, jijini Dar es Salaam iko mbioni kuanzisha Benki ya Akiba ya Maziwa, kuwasaidia wazazi wenye upungufu wa lishe hiyo kwa watoto wao. **PICHA: MTANDAO**

### YANAVYOHIFADHIWA

Dk. Mwanaidi anasema kwa kawaida mama atayekamua kutoa maziwa yake, bila ya kuweka katika friji, huweza kukaa kwa saa hadi nane pasipo kuathiriwa ubora wake na mtoto akayanywa.

Anasema, kwa mama ambaye ana maziwa yanayomtosha na ziada, atachangia benki na kwamba katika mfumo huo, itahitajika mashine za kuhifadhi ili yasiharibike kwa saa nyingi.

Daktari huyo bingwa, anaeleza asilimia 80 ya watoto wanaolazwa hospitalini hapo ni wazaliwa wa mahali hapo.

"Kwa kawaida maziwa ya mama yeyote hulingana, ila ubora huweza kutofautiana kutokana na lishe au mlo anaokula mama anayenyonyesha. Mama akishajifungua maziwa ya kwanza yana virutubisho vingi," anaeleza.

### UTAFITI ULIVYO

Dk. Mwanaidi anasema, utafiti walioufanya na kupokea maoni kuhusu kuanzishwa benki hiyo ikiwamo suala la utamaduni wa maeneo fulani, ilibainika asilimia 86 kwenye jamii ipo tayari kwa suala hilo.

Anasema, asilimia 93 walionekana iwapo wataelimishwa kuhusu benki hiyo, itasaidia kuepusha maambukizi kwenda kwa mtoto mwingine.

Daktari Mwanaidi anafafanua kwamba walibaini mama anayejifungua na kuumwa sana inasababisha mtoto kukosa maziwa ya mama yake, hivyo benki hiyo itawalenga watoto hao.

Daktari anaeleza watoto watakaonufaika na huduma hiyo ni wazaliwa wa hospitalini hapo, pamoja na mama ambao wako wodini, pia wanatoka nje ya hospitali, ili kuhakikisha usalama wa maziwa hayo.

"Kinamama wanaojifungua hapa ni asilimia 60 na hujifungia njiti na hawa watoto hawahitaji hata mlo wa milimita 20 ni wadogo mno, hivyo tuna uhakika maziwa yatapatikana kwa kina mama hawa, mengi tu yatabaki na kuwekwa benki," anasema.

Katika hilo, anataja matarajio yao ni kuanza kupatikana huduma hiyo kwenye maadhimisho ya Siku ya Unyonyeshaji Duniani, Agosti ijayo.

### KUTOKA UNICEF

Shirika la kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF) na washirika wake, linasema chini ya asilimia 50 ya watoto wachanga hunyonyeshwa katika saa ya kwanza ya maisha.

Licha ya kwamba, umuhimu wa mama na mtoto tangu kuzaliwa mtoto ngozi kwa ngozi ni muhimu na kunachangia kupunguza vifo vya watoto wachanga.

Aidha, kuna mwongozo wa unyonyeshaji bora wa watoto chini ya miaka miwili na kuna uwezekano wa kuzuia vifo vya watoto 800,000 kila mwaka.

Mwongozo huo unasema wanawake wanaoanza kunyonyesha katika saa ya kwanza baada ya kuzaliwa mtoto , kuna hatari inayopunguzwa ya kutokwa damu nyingi baada ya kuzaa.

Pia, unasema wanawake wanaoendelea kunyonyesha kwa muda wa miezi sita pekee, kunasaidia kutoona hedhi na kuhifadhi madini ya chuma mwilini.

AFYA

VITA VYA KIFUA KIKUU...

# Hospitali Kibong'oto ilivyoamua kupiga kambi mgodini Mirerani

- Mwingiliano tishio, hesabu wagonjwa balaa
- Ofisa Madini: Kinachojiri migodi yote kitaifa

**Na Mary Mosha,** SIMANJIRO

PENYE mashimo migodini kunatajwa chanzo cha magonjwa mbalimbali, ikiwamo kifua kikuu, unaosababishwa na bakteria, ukigusa athari za mapafu kwa kiwango kikubwa.

Ni maradhi yanayotajwa yanaweza kuathiri maeneo mengine mwilini. Kwa kawaida husambaa kutoka kwa mtu mmoja kwenda mwingine kupitia hewa chafu wanapokohoa, kupiga chafya, au mate hewani. Pia, kuna maambukizi mengi yasiyo na dalili wala madhara.

**MKURGENZI KIBONG'OTO**

Mkurugenzi wa Hospitali Maalumu ya Taifa ya Magonjwa ya Kibong'oto, Moshi Dk. Leonard Subi, anasema kwenye maadhimisho ya Siku ya Kifua Kikuu yaliyofanyika katika geti kuu Mgodi wa Mi rerani wilayani Simanjiro, Manyara, anasema wamelazimika kufanyia hapo hapo, kuhamasisha walio machimboni Mirerani, waangalie afya zao na kufanyiwa vipimo.

Anasema takwimu zinaonyesha asilimia 27 ya wagonjwa wanaolazwa hospitali Kibong'oto wanatoka kwenye machimbo ya madini na asilimia 70 wako katika hali mbaya, wakihudumiwa kwa mtungi wa hewa oksijeni.

"Kutokana na kubaini madhara makubwa yanayotokana na vumbi litokanalo na upasuaji miamba, madhara yanaweza kujitokeza baada ya wiki mbili, hadi miaka mitano. Hivyo basi, tuna kila sababu ya kuadhimisha maadhimisho hayo hapa Mirerani," anafafanua Dk Subi.

Pia, anaeleza utafiti unaonyesha wachimbaji wadogo wana uwezekano wa kuambukizwa mara saba zaidi ya mtu wa kawaida, sasa anawataka wasimamizi wa sheria na taratibu za afya na usalama kazini , waendelee kuwaelimisha wachimbaji.

"Elimu itapaswa itolewe kwa wachimbaji wakubwa, wadogo na wakati , pamoja na wamiliki wa migodi, ili waweze kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za mahali pa kazi, ili kudhibiti maambukizi ya kifua kikuu ambao inawapeleka Watanzania zaidi ya 70 kufa kila siku," anasema.

Dk. Subi anasisitiza ni ugonjwa unaotibika, unazuilika na unapona kabisa, takwimu zikionyesha hadi sasa jitihada zimefikia jamii kwa asilimia 64 tu na bado asilimia 36 ya wagonjwa wa kifua kikuu wapo ndani ya jamii.

Pia, ana maono kwamba, kila mgonjwa aliyepo kwenye jamii, ana uwezo wa kuambukiza watu kati ya 10 na 15, jambo lilil o hatari kwa wanajamii, sasa anawataka wajinusuru na hali hiyo.



Mkurugenzi wa Hospitali Maalumu ya Taifa ya Maambukizi Kibong'oto, Dk Leonard Subi akizungumza kwenye Maadhimisho ya Siku Kifua Kikuu Duniani, katika mgodi wa Mererani, wilayani Simanjiro. Wa kwanza kulia ni Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Simanjiro, Dk Aristide Rafael, pembeni yake ni Ofisa Mfawidhi wa Madini migodini Mererani, Justine Kababa. **PICHA: MARY MOSHA**

> **Bado watu wengi wanaopatwa na magonjwa hayo ni kutoka nchi nzima ya Tanzania, ambao baada ya kupata maambukizi hurudi maeneo ya familia zao na kuambukiza wengine, bila ya matibabu hadi kupoteza maisha.**

**DALILI ZAKE ZILIVYO**

Kuhusu dalili zake, Dk Subi anafafanua: "Miongoni mwa dalili za TB (kifua kikuu) ni pamoja na homa, baridi, kutokwa jasho usiku, kupoteza hamu ya kula, uchovu, kukonda, kupungua uzito na wakati mwingine kucha kujikunja pembeni, kukohoa kwa wiki mbili mfululizo.

"Unapoona dalili kama hizi mpeleke mtu huyo katika kituo cha afya kwa uchunguzi zaidi na matibabu yote ni bure, na ndani ya saa mbili itaweza kugundulika na kuanza dawa, na dawa ni bure na zinapatikana nchi nzima," anadokeza, kwamba serikali imeshaelekeza fedha myingi kukabili maradhi hayo,ikijumuisha ununuzi wa mashine bora za upimaji.

"Upimaji huo ni bure na unafanyika kila kituo cha afya na yanafanyika nchini nzima na kutokana na 'usasa' wa mashine na vitendea kazi, muda umepungua kutoka siku mbili au tatu hadi saa mbili unakuwa umeshapata majibu yako na kuanzishiwa dawa," anafafanua.

Dk. Suni anatoa angalizo kwamba ushindi kukabiliwa ugonjwa huo unaanza na kuwahi matibabu, akifafanua: "Mazingira ya vituo vyetu vya afya yameboroshwa, Hakuna kunyanyapaliwa na mazingira, wala wahudumu wa afya, dawa zipo kwa asilimia 100 na hakuna mgonjwa yeyote atakayekosa dawa popote alipo."

**KIBONG'OTO VITANI**

Anasema Hospitali ya Kibong'oto, ina gari maalum la kuhudumia wachimbaji, kwa huduma zote za kihospitali hukohuko katika maeneo yao.

"Licha ya matibabu hayo kutolewa bure kwa waathirika, lakini matibabu hayo yana gharama kubwa. Kila siku hospitali kwetu tunapata wagonjwa 20 hado 30 wanatumia hewa tiba (Oxygen), yanayogharimiwa na serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, ndio maana tunasema tuwekeze kwenye kuzuia zaidi," anaeleza.

Wachimbaji wengi ni vijana na sehemu kubwa wanalala kwenye misongamano, hivyo anaona ni wajibu wa kila mmoja kuchukua tahadhari ya kukabili mazingira hatarishi ya kifua kikuu.

Dk. Suni anaainisha hospitalini Kibong'oto asilimia 90 ya wanaougua kifuu kikuu cha kawaida wanatibiwa na kupona, vivyo hivyo kwa asilimia 75 ya kifua kikuu sugu wanapona.

**ULINGO WA MADINI**

Justine Kababa ni Mwakilishi wa Ofisa Madini wa Mgodi wa Mirerani, anasema katika eneo hilo kunakadiriwa uwapo wa mwingiliano wa watu kati ya 10,000 na 15,000 kila siku ndani ya migodi zaidi ya 830.

Anaeleza kina cha machimbo hayo yamezama umbali wa mita 1800 (kilomita 18), hali inayoonyesha hatari za kiafya na hasa kukosekana hewa ya kutosha.

"Kutokana na hali hiyo, tunaweza kuona watu wanaoumwa ni wengi. Tunaomba mnapokuja tena tukae na vyombo vya usalama kuona namna ambavyo mnaweza kuingia na kufanya upimaji wa watu wote, ili waathirika waweze kuanzishiwa dawa," anasema Kababa.

"Tutumie siku hii katika kuhamasisha watu hao kujitokeza kwa wingi katika kupima na kutambua afya zao," anapendekeza.

Mwakilishi wa jamii hiyo machimboni, Moses Komba, anasema kuwapo hali mbaya na hatari, inaonyesha dira kuu ya hatari inayowaangukia vijana kwa asilimia 90.

"Bado watu wengi wanaopatwa na magonjwa hayo ni kutoka nchi nzima ya Tanzania, ambao baada ya kupata maambukizi hurudi maeneo ya familia zao na kuambukiza wengine, bila ya matibabu hadi kupoteza maisha," anafafanua.

Komba anataja maeneo mengine yenye athari kwa kifua kikuu ni machimbo ya Ulanga, pia kwenye mikoa ya Singida na Tabora, janga likiwaangukia zaidi vijana.

"Zipo sheria za uchimbaji, Ninaamini zikiwekewa mkazo, zinaweza kupunguza tatizo hili, kwa kuhakikisha kila mtu amefuata sheria, taratibu na kanuni kwanza kwa wamiliki wa migodi, wachimbaji wakubwa na hata wadogo," anaeleza Komba.

**DAKTARI WA SIMANJIRO**

Dk Aristide Rafael, Mganga Mfawidhi wilayani Simanjiro, anasema ni kati ya wilaya zilizoathirika sana na kifua kikuu, akitaja mwaka jana, zaidi ya wagonjwa 500 waligundulika, ambao ni sawa na asilimia 96 ya lengo walilopewa.

Anasema mgodini Mererani peke yake, walikuwapo wagonjwa 245 sawa na asilimia 45 na kati yao, 12 wastani wa robo walikuwa na kifua kikuu sugu. Mchimbaji madini, Kulwa Honest, anakiri kuwapo matatizo mengi wanayokabiliana nayo machimboni, kwa sababu wanapigana kutimiza mahitaji yao kiuchumi.

"Tumeacha familia zetu huko, tupo kwa ajili ya utafutaji na muda mwingi tupo chini kwenye machimbo, hali kama hiyo inatupelekea kukodi chumba tukalala hata sita, hivyo kama kweli kutakuwa na mtu kaadhirika ni rahisi kuambukizwa," anasema

Felix Eusabian ni mchimbaji mdogo, anafafanua kwamba elimu ieendelee kutolewa na watu wabadilike kwa kujitokeza kupima afya zao, akitaja mafanikio "kwa sasa hata zile nguo za vumbi tunaziacha humu ndani ni tofauti na zamani."

AFYA

# Wataalamu afya: Kunusuru macho ya mtoto mpiganie miaka minne hadi tisa

**Na Beatrice Philemon**

• Waeneza ujuzi shuleni wasaidiwe udhibiti

UNAPOZUNGUMZIA magonjwa ya macho yanayoleta upofu kwa watoto katika umri mdogo, si wazazi wote nchini wanaofahamu fika aina zake na jinsi ya kupata huduma ya matibabu ya macho.

Magonjwa hayo ni mkusanyiko wa maradhi ya aina mbalimbali yanayoweza kusababisha hali ya upofu kwa watoto walio na umri wa miaka 16 au chini ya hapo. Inaelezwa uchunguzi wa kila mara wa macho ya mtoto, unaweza kutambua matatizo ya uono huo mapema.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi Mkazi wa Shirika lisilo la kiserikali, Vision Care Tanzania, Jihye Kim, anasema utambuzi wa ugonjwa wa macho kwa watoto unapofanyika mapema, ni njia bora kumsaidia kuepuka upofu, kupata matibabu mapema, pia humsadia kufaulu vizuri katika masomo yake darasani.

Matokeo bora zaidi darasani yanatajwa yanatokana na matibabu yaliyoanza kabla ya umri wa miaka minne, pia matokeo mazuri yanaweza kupatikana ikiwa hatua itachukuliwa kabla ya umri wa miaka tisa kwa mtoto husika.

Ili kuzuia upofu na kusaidia watoto wasome vizuri, shirika hilo hivi karibuni limefanya uchunguzi kwa wanafunzi wa shule za msingi na awali katika wilaya ya Kibaha, kugundua wanafunzi wenye matatizo ya macho, ikiwamo uoni hafifu kama vile kuona kwa shida kwa karibu na mbali.

Jumla ya wanafunzi 2,250 kutoka shule tatu zikiwemo Tumbi, Kambarage za wilaya ya Kibaha, walifanyiwa uchunguzi wa macho na kati yao wanafunzi 100 waligunduliwa kuwa na magonjwa ya macho ya aina mbalimbali.

Kim anasema,watoto wote waliogunduliwa kuwa na matatizo ya macho, watapatiwa matibabu bure hospitalini, ikiwamo katika Hospitali ya Rufani ya Tumbi.

"Lengo letu ni kufikia wanafunzi 3500 kwenye shule tano za msingi katika wilaya ya Kibaha. Lakini hadi sasa tumefanikiwa kufikia wanafunzi 2,250 katika shule tatu, wakiwamo wanafunzi wa awali," anasema.

Pia, asasi hiyo ya Vision Care Tanzania. imefanikiwa kutoa mafunzo kwa jumla ya walimu 62 wa shule za msingi, jinsi ya kugundua matatizo au magonjwa ya macho kwa wanafunzi, kupima macho na kuangalia viashiria vya ugonjwa wa macho.

Inafafanua kwamba, sababu kubwa ni walimu wanakaa muda mrefu na wanafunzi hata inakuwa rahisi kwao kubaini mapungufu waliyo nayo.



Mratibu wa Huduma za Macho Wilaya ya Kibaha, Sarah Mghwira, akimfanyia uchunguzi wa macho mtoto wa darasa la awali. **PICHA ZOTE: BEATRICE PHILEMON**



Mwalimu wa Darasa la Awali, katika shule ya Msingi Tumbi, akimpima urefu mtoto wa darasa la awali, Mevati Zuberi, kabla ya kwenda kupima macho.

### WALIMU WAPEWA UJUZI

Akizungumza na Nipashe, mwalimu wa darasa la nne katika Shule ya Msingi Tumbi, Alice Kaguo anasema kupitia mafunzo na ujuzi alioupata, kutoka kwa wataalamu wa Vision Care Tanzania,

"Mafunzo haya yamenisaidia kujua kama nina shida ya macho au mwenzangu ana shida ya macho ili aweze kwenda hospitali kupata matibabu," anasema Mwalimu Alice.

Pili, yamemsaidia kujua wanafunzi wenye matatizo ya macho shuleni, pia hata kama kwenye familia sasa hivi mtu akiwa na shida ya macho nitaweza kumsaidia na kumpa ushauri na kwenda kwa wataalamu kupata matibabu zaidi.

"Sasa hivi nimeanza kutoa elimu hii kwa wanafunzi shuleni. Kwa mfano niliona mtoto shuleni ana macho mekundu, nikamuuliza mbona jicho jekundu? akasema linauma, baadae nilimshauri kwenda hospitali kupata matibabu," anasema.

Anashukuru Asasi ya Vision Care Tanzania kwa kutoa mafunzo yanayowasaidia waelimishaji darasani, kugundua watoto wenye magonjwa ya macho na hatimaye wanapewa ushauri na kupata matibabu mapema, kabla hajaathirika zaidi. Pia, walimu hao walipata nafasi ya kujaribu stahi zao za kuwapima wanafunzi, kuanzia waliopo katika shule ya awali hadi darasa la saba.

"Kabla ya kupata mafunzo, nilikuwa sijui jinsi ya kutambua watu wenye matatizo ya macho. Zamani nilijua viashiria vya jicho kuuma ni mpaka... kwa kuangalia," anasema.

Baada ya mafunzo, anasema amegundua jicho linaweza kuonekana zima kwa kuliangalia, ila likimulikwa tochi au kifaa cha 'Vision Test Chart' inagundilika shida yake.

Rai ya mwalimu huyo, mafunzo hayo yaendelee kutolewa kila mara kuwasaidia walimu wawe na kumbukumbu sahihi. Anafafanua:"Watoto pia wapewe elimu ya afya ya macho na wao watakuwa mabalozi wazuri kwenye maeneo yao wanayoishi."

Anaeleza umuhimu kuwafundisha watoto namna inayowarahisishia kuwagundua wenzao, hata wakijua matatizo yanayowasibu, wakati huohuo wanakuwa na weledi wa kuwagundua wenzao wenye matatizo ya macho, hata wakawasaidia.

Mwalimu wa Afya Msaidizi, katika Shule ya Msingi Tumbi, Magreth Msoka anasema alipata mafunzo jinsi ya kugundua matatizo kwa watoto na namna ya kujifunza darasani, kutokana na wanayofunzwa.

"Elimu hii imenisaidia kugundua matatizo ya macho kwa watoto, namna ya kuwasaidia watoto wenye matatizo ya macho.

"Kwa mfano, kuna watoto ambao walikuwa hawana uwezo wa kuona vizuri katika kujifunza , niliwasaidia kukaa mbele ili waweze kujifunza kwa urahisi zaidi," anasema Anasema katika darasa lake kulikuwapo wanafunzi watatu ambao amewasaidia kupata matibabu hospitalini na sasa wamepatiwa miwani.

"Hivi sasa wanafanya vizuri darasani baada ya kupatiwa huduma ya dawa na miwani, kati ya wanafunzi hao wawili wapo darasa la saba na mmoja darasa la sita," anaeleza

Mwalimu Magreth anahimza kamba elimu bado inahitajika sana na hasa kwa wazazi, kwani kuna changamoto upande huo.

"Sisi tunaweza kumsaidia mtoto kupata dawa na hata miwani, lakini mtoto akienda nyumbani unakuta mzazi anamwambia mtoto asivae miwani au kama amepewa dawa asimeze , hili ni tatizo kubwa sana," anaeleza.

"Nimeweza kuhamasisha majirani zangu kwenda kupima afya ya macho,: anahitimisha mwalimu huyo wa afya.

**"Sisi tunaweza kumsaidia mtoto kupata dawa na hata miwani, lakini mtoto akienda nyumbani unakuta mzazi anamwambia mtoto asivae miwani au kama amepewa dawa asimeze, hili ni tatizo kubwa sana.**

AFYA

# Mwenye ulemavu awapa moyo wenziwe kutumia simulizi yake

• Polio ‘ilimmaliza’, baba naye akafariki • Wote wakakata tamaa, mama asema hapana • Shule ikawa kila kitu, leo bosi serikalini



Washiriki mkutanoni wakipata darasa la Oliver Njogopa. **PICHA ZOTE: CHRISTINA MWAKANGALE**

**Na Christina Mwakangale**

UTAMBUZI wa mapema wa watoto wenye ulemavu na kuwapa nafuu stahiki ikiwamo huduma ya utengamao, ni kati ya vipaumbele vya serikali, ikibainisha kwamba inasaidia kupunguza makali ya ulemavu ukubwani au kuwaondolea kabisa adha.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mwandamizi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu- Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Oliver Njogopa, anafafanua zaidi yale aliyopitia maishani mwake, akikumbuka alivyougua ugonjwa wa polio tangu umri wa miaka miwili.

Oliver, anayetumia magongo kumsaidia, anasimulia hayo akiwa mgeni rasmi kufungua mkutano wa kutathmini masuala ya kijinsia na ujumuishaji wa watu wenye ulemavu katika mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan, uliofanyika hivi karibuni mkoani Dar es Salaam.

Akitumia uzoefu wa yaliyomkuta, anawaasa wanajamii wasiwatenge watu wenye ulemavu pamoja na kuondokana na dhana kwamba uwezo wao ni mdogo, akisema hadi kufikia hatua aliko ni kutokana na elimu aliyoipata, mpambanaji mkuu akiwa mama yake mzazi.

“Nilipata ulemavu katika umri wa miaka miwili baada ya homa kali ya Polio, miaka ya 1970. Sikuweza kukaa hadi nisaidiwe, nilipooza kuanzia kiunoni hadi miguuni, nilisimuliwa,” anaeleza Oliver.

“Mapema tu wazazi wangu walinipeleka hospitali, nikalazwa MOI (Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu) miezi sita na nilifanyiwa mazoezi kila mara. Watoto wa familia yetu, pia walielekezwa namna ya kunifanyisha mazoezi,” anasema Oliver.

> **Kwa kweli nilichukia sana, ila nimebaini mama aliangalia mbali juu yangu. Watu wenye ulemavu elimu inaweza kutukomboa, tujiamini.**



Oliver Njogopa, akizungumza mkutanoni , akiwapa darasa wenye ulemavu.

Anasema kutambuliwa mapema hali yake na kufikishwa kwenye matibabu, ilichangia kupunguza madhara na kumsaidia kusonga mbele na kupata elimu, ingawa alianza kutembea akiwa na miaka minne.

“Nilichimbiwa shimo ili miguu itumbukie ndani na nisimame kwa muda mrefu. Baba yangu alifariki nikiwa na umri wa miaka miwili, umri huo huo ambao niliugua. Jamaa zangu baadhi wakadai Oliver, akae tu nyumbani ni mlemavu,” Oliver anaeleza hayo.

Huku akiwapa matumaini wengine wenye ulemavu ama kwa kuzaliwa au kuupata baada ya kuzaliwa, Oliver anasema silaha kubwa kwa watu wa kundi hilo, ni elimu.

“Mama yangu alinipigania nikasoma. Mama alinichapa sana iwapo nilifanya vibaya masomoni. Jicho lote lilikuwa kwangu zaidi na kuwaacha ndugu zangu watatu.

“Kwa kweli nilichukia sana, ila nimebaini mama aliangalia mbali juu yangu. Watu wenye ulemavu elimu inaweza kutukomboa, tujiamini,” anasimulia Oliver, akiongeza:

“Kuwapo ombaomba mlemavu anayeomba barabarani sababu kuu ni kutoendelezwa kielimu, elimu fursa muhimu.”

Anasema jamii iendelee kuwafichua watoto ambao wanakoseshwa fursa ya elimu kutokana na ulemavu wao, akisema: Nikiwa Shinyanga tukiandaa mwongozo uliopo sasa, nilikutana na mtoto ana ulemavu wa miguu, ila misuli yake iko vizuri

“Niliongea na CCBRT akafanyiwa upasuaji sasa amenyanyuka, ingawa kwa fimbo, lakini kuinuka ni hatua kubwa anapata fursa zingine,” anaeleza

**MKAKATI WA SERIKALI**

Oliver anasema katika kipindi cha mwaka mmoja, kwenye Mpango wa Kuwatambua Mapema Watoto wenye Ulemavu kwa Kupata Afua na Utengamao, ilibanika watoto 28,698 katika kata 3,785 wana mahitaji maalumu ila kiwazo ni kufichwa ndani na walezi au wazazi wao.

Afua kimsingi, ni mchangayiko wa jozi ya mahitaji ya huduma za kitabibu. Oliver anasema ni mpango uliozinduliwa mwongozo wa taifa wa utambuzi wa mapema na afua stahiki kwa watoto wenye ulemavu, Desemba mwaka jana.

**UGONJWA POLIO**

Polio ni ugonjwa unaoathiri mfumo wa mishipa na unaweza kusababisha udhaifu wa ama misuli au kupooza na kumsababishia mtu kushindwa kusogeza misuli.

Ugonjwa huo ulienea sana katika miaka ya 1970 na kabla ya hapo, ingawa ni adimu, chanjo imepunguza uwepo wa virusi. Polio hutokea zaidi kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Watu ambao bado hawajapata chanjo wapo kwenye hatari ya kuambukizwa.

Virusi vya polio husambazwa kutoka mtu mmoja hadi mwingine. Polio inasambazwa kwa kukohoa, kupiga chafya au kugusa kinyesi.

Mara chache sana kuwapata watu waliopata chanjo, huweza kuwapata wale ambao hawajachanjwa virusi vya polio.

Dalili zake huweza kujumuisha homa, koo kuuma, maumivu ya kichwa na misuli kuuma. Baadhi ya watu hupata udhaifu wa misuli.

Maambukizi ya polio hayawezi kutibiwa, kawaida hudhibitiwa dalili tu. Matokeo baada ya maambukizi yake hutegemea dalili ni kali kiasi gani. Inawezekana hata kusababisha ulemavu wa kudumu na kifo.

Matibabu hulenga kupunguza dalili. Dawa za maumivu huweza kutolewa kwa ajili ya maumivu ya kichwa na misuli na watu wenye udhaifu wa misuli unaoendelea huweza kuhitaji, ili kusaidia kuboresha nguvu ya misuli.

Ikiwa misuli ya kupumua imeathirika na kuwa dhaifu, mashine huweza kuhitajika ili kumsaidia aliyethirika kupumua.



## Wapewa angalizo ujenzi wa makazi maeneo hatarishi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imewataka wananchi kuepuka kujenga katika maeneo hatarishi yanayoweza kusababisha maafa kama vifo, uharibifu wa miundombinu na mazingira..

Angalizo hilo lilitolewa na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge na Uratibu, Kaspar Mmuya, wakati akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Usimamizi wa Maafa kilichokutanisha Makatibu Wakuu wa Wizara ambazo ni wadau wa usimamizi wa maafa na wataalamu kilichofanyika jijini Dodoma.

Naibu Katibu Mkuu huyo alisema kuwa ipo haja ya wananchi kupewa elimu kupitia wataalamu kuhusu dhana ya usimamizi wa maafa na namna ya kuzuia madhara ya maafa au kuchukua hatua ya kujiokoa yanapotokea.

"Tunahimiza tufuate maelekezo ya wataalamu kwa kutojenga kwenye maeneo ambayo hayafai hasa ya mabondeni, kujiepusha na kulima maeneo ya vyanzo vya maji na wafugaji kutokuwa na mifugo mingi ambayo anashindwa kuihudumia hatimaye tatizo likitokea la ukame anashindwa kuwapa huduma bora,"alisema Mmuya.

Aidha, aliwataka wakulima nchini kuzingatia pia utabiri wa hali ya hewa ambao umekuwa ukitolewa na wataalam ili kujua mazao rafiki ya kulima kwa msimu husika.

"Tuangalie mabadiliko ya hali ya hewa tuweze kulima kulingana na hali ya hewa na elimu hii itatolewa kwa wakulima kama kipindi cha mvua nyingi tunatakiwa kulima nini na wakati wa mvua chache tulime nini elimu hii itatolewa maeneo yote,"alieleza.

Kuhusu sera alibainisha kwamba ofisi hiyo kama wasimamizi wa sera na wasimamizi wa maduhuli katika kila wizara hazina budi kuweka bajeti itakayosaidia kukabili changamoto zinazotokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

"Kwa sisi wasimamizi wa sera na waduhuli katika kila wizara kujaribu kuweka bajeti kila wizara ili tatizo linapojitokeza tuwe na mpango wa muda mfupi kutekeleza changamoto zinatokana na mabadiliko ya hali ya hewa," alibainisha Mmuya.

Mkurugenzi wa Idara ya Menejimenti ya Maafa Ofisi ya Waziri Mkuu, Meja Jenerali Michael Mumanga, alisisitiza sekta mbalimbali zinazohusika na uhifadhi wa chakula na uokoaji kuweka mikakati thabiti itakayosaidia kudhibiti maafa na kuyakabili pindi yanapojitokeza.

# UNICEF yashtushwa wingi watoto wasiokwenda shule

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

PAMOJA na jitihada zinazofanywa serikali kuboresha na kuinua elimu nchini takwimu za elimu bado zinaonyesha idadi kubwa ya vijana na watoto wenye umri wa kuwa shule hawapo shuleni imebainishwa.

Kaimu mkuu wa kitengo cha elimu kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) Ayoub Kafyulilo, alibainisha hayo alipokuwa akitoa hotuba yake kwenye hafla ya kufunga mafunzo ya ujuzi mbalimbali kwa walimu wawezeshaji,walimu wenye ulemavu, wanafunzi katika fani za TEHAMA,ufundi na ujasiriamali.

"Ndugu mgeni rasmi kwa niaba ya UNICEF, napenda nitumie fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa serikali ya Tanzania kwa jitihada kubwa inazofanya kuwekeza katika sekta ta elimu.

"Tunatambua jitihada kubwa zinazofanywa hivi sasa katika kupanua na kuboresha elimu ya ufundi, tunaona jitihada zinazofanywa kwenye ujenzi wa madarasa nakuendelea kutoa elimu bila malipo hongereni sana"alisema

Aidha, alisema pamoja na jitihada kubwa serikali inazofanya kuboresha elimu na kuinua sekta hiyo takwimu zinaonyesha idadi kubwa ya vijana na watoto wenye umri kuwa shule hawapo shuleni.

"Utafiti uliofanywa na wizara ya elimu mwaka 2016 ulionyesha kwamba zaidi ya watoto milioni 3.5 wenye umri wa kuwa shuleni, hawakuwepo shuleni.

"Utafiti mwingine uliofanyika mwaka 2021 na wizara ya elimu pia umeonyesha bado kuna idadi ya watoto na vijana wapatao milioni 3.2 wenye umri wa kuwa shule lakini hawapo shuleni na idadi kubwa ya hawa vijana waliokosa fursa ya elimu au hawakufanikia kuendelea na masomo baada ya elimu ya msingi au sekondari hawana ujuzi wa kuwawezesha kujitegemea"alisema

Vilevile, alisema kwa kutambua changamoto hiyo UNICEF kwa kushirikiana na taasisi ya elimu ya watu wazima ilianzisha program ya MECHAVI, mpango wa elimu changamani kwa vijana au kwa kingereza (IPOSA). Ikiwa na lengo la kutoa stadi za ufundi wa awali, ujasiriamali,stadi za maisha na kisomo kwa vijana wenye umri kati ya miaka 14 hadai 19 ambao walikosa fursa ya elimu ya msingi na sekondari.

"IPOSA ilizinduliwa mwaka 2019 na tayari vijana 30,000 wameshanufaika na mpango huu na wengine 5,000 wamepewa vyeti vya utambuzi kutoka taasisi ya elimu ya watu wazima"alisema

Hata hivyo, alisema programu hiyo imelenga kuwafikia vijana walio katika mazingira magumu na wenye uhitaji wa ujuzi katika mikoa nane Tanzania bara.



Meneja wa NMB Kanda ya Kaskazini, Dismas Prosper (kulia), akikabidhi pikipiki ya miguu mitatu maalumu kwa ajili ya kubebea mizigo aina ya Skymark, Ally Athumani Mnyone, baada ya kuibuka mmoja kwa washindi wa kampeni ya bonge la mpango iliyoendeshwa na benki hiyo, jijini Tanga juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kasi utoaji chanjo UVIKO-19 kuongezeka

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imejipanga kuongeza kasi ya uchanjaji chanjo ya UVIKO-19 katika jamii ili kufikia lengo la idadi ya asilimia 70 ya watu walio katika umri wa kuchanja kupitia msaada wa Dola za Marekani milioni 25.

Kiasi hicho cha fedha kilitangazwa hivi karibuni kwenye kikao kilichofanyika Machi 3, 2022 kati ya Rais Samia Suluhu Hassan na Balozi Samantha Jane Power, msimamizi Mkuu wa Shirika la Kimataifa la Msaada la Marekani (USAID).

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alibainisha hayo wakati alipotembelewa na Balozi wa Marekani nchini Dk. Donald Wright katika Ofisi za Wizara jijini Dodoma.

Ummy alimshukuru Balozi huyo baada ya Serikali ya Marekani kuipatia Tanzania Dola za Kimarekani Milioni 25 kupitia Mpango wa Serikali ya Marekani wa Global Vax ambao unalenga kuchangia kufikiwa kwa lengo la kuchanja chanjo ya UVIKO-19 kwa asilimia 70 ya watu ifikapo Desemba, 2022.

Aidha, waziri Ummy alisema fedha hizo zitatumika katika kuhamasisha makundi yaliyo hatari ya kuambukizwa UVIKO-19 pamoja na makundi mengine yanayolengwa kufuatia kutofikiwa kwa malengo ya uchanjaji yaliyowekwa.

"Tutatumia ushawishi kwa viongozi wa ngazi zote na jamii kwa ujumla kupitia mikusanyiko na pia tunatarajia kuongeza idadi ya huduma za chanjo za mkoba karibu na jamii. Kwetu itakua ni sehemu nzuri ya kutoa elimu ya kuhamasisha kuhusu chanjo," alisema Waziri Ummy.

Alisema Tanzania sasa ina chanjo ya UVIKO-19 inayoweza kuchanja watu takribani milioni sita huku akiongeza kuwa fedha hizo zitasaidia kufikia lengo la kuchanja asilimia 70 ya watanzania.

Aidha, Waziri Ummy alimwambia Balozi Donald kuwa hivi sasa wizara ya Afya imejikita katika kuimarisha huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja kuboresha huduma za mama na mtoto na kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Balozi Dk. Donald alisema serikali yake iko tayari kushirikiana na Tanzania katika mapambano dhidi ya magonjwa ya kuambukiza na yasiyokuambukiza, huku akisisitiza serikali ya Marekani itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kutoa elimu kwa jamii ili kujikinga na magonjwa.



# Wasichana waeleza sababu ya kutoa mimba kiholela

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

NUSU ya wanawake wanaolazwa katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya wanadaiwa kusumbuliwa na maradhi yanayotokana na utoaji holela wa mimba hasa unaofanyika mitaani bila kuzingatia utaalamu.

Kati ya wanawake 50 wanaolazwa katika hospitali hiyo, 25 wanakabiliwa na matatizo hayo ambayo yanatokana na utoaji wa mimba hali inayoashiria ongezeko la utoaji mimba holela.

Mabinti wenye umri wa kuanzia miaka 15 hadi 25 ndiyo wanaolazwa katika hospitali hiyo kwa sababu ya kutoa mimba kwa njia zisizokuwa salama.

Akizungumza na Nipashe, Daktari Bingwa wa magonjwa ya kinamama katika hospitali hiyo, Dk. Soter Levasha, alisema kila mwezi wanapokea mabinti wenye tatizo la kutoa mimba.

Alisema wanafika katika hospitali hiyo wakiwa tayari wameshatumia dawa za kutolea mimba mitaani ambazo haziwasaidii badala yake zinawasababishia madhara kiafya na damu kuvuja na kuhatarisha afya zao.

"Kila mwezi tunapokea binti wanaotoa mimba huko mitaani wanakuja wakiwa na hali mbaya, licha ya kwamba hakuna kifo kilichoripotiwa kwa kipindi hiki cha kuanzia Januari hadi Machi, lakini mabinti watatu tuliwawekea uniti za damu kutokana na kuvuja damu baada ya kujaribu kutoa mimba huko mitaani, alisema Dk. Levasha.

Alisema ziko athari mbalimbali zitokanazo na utoaji wa mimba kwa mabinti ikiwamo, ugumba, kansa na vifo.

Alisema alipowadadisi mabinti hao sababu ya kutoa mimba walisema wenza wao ambao ni waume za watu hugoma kulea na hulazimika kutoa ili kuendelea na maisha yao.

"Mabinti wengi wanabeba mimba za waume wa watu ambao wanapoelezwa kwamba wamebeba ujauzito wanasema hawako tayari kulea hizo mimba hivyo huwalazimu kutoa jambo ambalo linahatarisha afya za mabinti hao," alisema Dk. Levasha.

Aliwaomba wanaume walifikia umri wa utu uzima kuacha kuharibu ndoto za mabinti na badala yake wawalinde ili nao baadaye waolewe kisha kuwa na familia zao.

Baadhi ya kinamama wa Jiji la Mbeya, wamesema sababu kubwa inayochangia kutoa mimba ni wenza wao kugoma kuhudumia mimba na mtoto na kwamba kutokana na ugumu wa maisha wanalazimika kufanya hivyo.



Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, Reuben Mfune, akizindua zoezi la uwekaji wa anuani za makazi katika Mtaa wa Relini, Kata ya Lugelele, wilayani humo juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Msako wa nyumba kwa nyumba watoto wasioenda shule waanza

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

MKUU wa Wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Magereza, Ismail Mlawa, ametangaza kufanya msako wa nyumba kwa nyumba kuwabaini wazazi pamoja na walezi ambao hawajawapeleka watoto shule kuanza masomo ya kidato cha kwanza.

Mlawa alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na Nipashe kuhusu mwitikio wa wazazi kuwapeleka shule watoto wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza.

Alisema hadi sasa wanafunzi 327 kati ya 5,461 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza hawajaripoti shule na kutoa muda wa wiki moja kuanza shule.

"Tangu Aprili 2 nilitoa agizo kwa wazazi na walezi wa watoto wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kuanza masomo mara moja na kwamba dhamana hiyo imebebwa na wazazi wakikaidi watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria," alisema Mlawa.

Alisema serikali imejitahidi kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa pamoja na samani, lakini baadhi ya wazazi bado hawajapeleka watoto shule jambo alilosema halitavumilika.

Alisema katika Wilaya ya Kyela jumla ya vyumba 67 vya madarasa vimejengwa kupitia fedha za UVIKO-19 na kwamba hakuna uhaba watoto wote watasoma kwa utulivu.

"Kesho ndiyo mwisho kwa wazazi kuwapeleka watoto shuleni, baada ya hapo tutaanza msako wa nyumba kwa nyumba kuwabaini waliokaidi na kisha kuwashughulikia kwa mujibu wa sheria," alisema Mlawa. Katika taarifa yake, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Katule Kingamkono, alisema Baraza la Madiwani halijafurahiwa na kitendo cha baadhi ya wazazi kutowapeleka watoto shule wakati serikali imejitahidi kuweka mazingira rafiki kwa ajili ya kusomea.

## Vijana wahamasishwa kuchangamkia fursa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

VIJANA mkoani Mbeya wameshauriwa kuchangamkia fursa mbalimbali zinazojitokeza kupitia mashirika na taasisi ili kujikwamua kiuchumi badala ya kujiingiza kwenye makundi yasiyofaa na kuharibu ndoto za maisha yao.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mkurugenzi wa Rafael Group, linalojihusisha na uuzaji na usambazaji wa nafaka mbalimbali jijini Mbeya, Rafael Ndelwa.

Alisema ili vijana waweze kutimiza malengo yao, lazima kuheshimu ndoto za maisha yao badala ya kushawishika na wenzao na kujiingiza kwenye makundi yasiyofaa.

"Mimi ni miongoni mwa vijana wa mfano mkoani Mbeya, nilianza kufanya shughuli ndogo kabisa za uuzaji wa usambazaji wa nafaka, nilikuwa na mtaji mdogo, lakini kwa kuwa nilikuwa na maono ya kufika mbali nilihakikisha natimiza azma yangu ambayo imenisaidia sasa namiliki kampuni kubwa ambayo pia imeajiri vijana wengi," alisema Ndelwa.

Alisema kwa sasa kampuni yake ina uwezo wa kukopesha pembejeo za kilimo wakulima wa mazao kama vile maharagwe mpunga, ngano na baada ya mavuno wakulima hao humpatia mavuno kulingana na gharama za pembejeo zilizotolewa.

Alisema zaidi ya wakulima 100 wamenufaika na fursa hiyo na kumuwezesha yeye kuwa na akiba ya mazao mengi ambayo huyachakata kisha kuuza ndani na nje ya nchi.

Pia, alisema ameweka mashine kubwa za kisasa kwa ajili ya kusaga nafaka za mpunga katika kampuni yake na kuyapaki kwenye vifungashio vyenye nembo ya kampuni yake.

Aliwashauri vijana kuchangamkia fedha za asilimia 10 za mikopo inayotolewa na halmashauri kwa kuhakikisha wanajiunga kwenye vikundi ili waweze kukopesheka na kuanzisha shughuli za kujikwamua na umaskini.

Kwa upande wake, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya, Suma Fyandomo, alisema katika kuhakikisha wananchi wa mkoa huo wanafanya shughuli zao wakiwa na afya, alitoa Sh. milioni 15 kwa ajili ya kuwakatia bima wananchi 500.

Alisema bima hizo ni kuhakikisha wananchi wanapata matibabu bila kikwazo ili waendelee na shughuli zao za uzalishaji mali bila tatizo.





## SMZ yajitosa malalamiko watendaji kutowajibika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Muhammed Said, amesema amepokea malalamiko ya wananchi wa Mji Mkongwe kuhusu kutowajibika kwa baadhi ya watendaji wa Mamlaka ya Mji Mkongwe.

Alieleza kuhusu suala hilo wakati akizungumza na waandishi wa habari jana baada ya kusikiliza malalamiko ya wananchi na wafanyabiashara wa Mji Mkongwe hapo Forodhani Mjini Zanzibar.

Alisema wananchi wamemlalamikia kukosa vibali vya ujenzi kwa ajili ya matengenezo ya nyumba zao katika mji huo ambao ni urithi wa dunia.

Alikiri kuwepo kwa tatizo hilo kwa baadhi ya watendaji kutowajibika na kuahidi kuwa atalifanyia kazi ili kila mmoja kwa nafasi yake kuwajibika.

Alisema lazima urithi wa mji huo kuenziwa na kuthaminiwa ikiwemo mazingira safi ya mji huo ambao ni miongoni mwa vivutio vya kitalii.

Katika hatua nyingine, Simai alisema iko haja ya kuzifanyia kazi sheria zilizopo kwa miaka mingi katika matumizi ya njia za Mji Mkongwe ambapo zamani watu waliziheshimu kwa kuendesha baiskeli kule tu wanakoruhusiwa tofauti na sasa ambapo wanapuuza na kila njia imekuwa ruhusa mtu kupita apendavyo bila kujali marufuku iliyowekwa.

Waziri huyo alieleza kuwa, dhamira ya wizara yake ni kumfanya kila mkaazi wa Mji Mkongwe awe mlinzi katika kuhakikisha unatunzwa kiusafi, kiusalama na heshima kwa wageni, pamoja na kudhibiti mambo na vitendo visivyotakiwa ndani ya mji huo.

Aliahidi kuyapitia maoni yote na ushauri uliotolewa na wananchi, akisema anaamini bado wanapenda mji huo uendelee kuwemo kwenye urithi wa kimataifa ili UNESCO iongeze nguvu katika kusimamia ukuaji na ustawi wake.

Baadhi ya wananchi wa mji huo, walidai kupigwa danadana zisizokwisha katika kufuatilia haki zao za majengo waliyosema wanayamiliki kihalali na kisheria.

Wengine wamelalamikia baadhi ya majirani zao kufanya shughuli za ujenzi ambao pia unaathiri nyumba zao kwa kupasuka nyufa zinazoziweka katika hatari ya kuporomoka.

Salma Maulid mkaazi wa mji huo, alisema tokea mwaka 2009 amekuwa akihangaika katika mamlaka za serikali kutaka haki itendeke baada ya jirani kuingilia na kujenga ndani ya himaya yake hali inayomzuia kutumia kwa uhuru sehemu ya nyumba anayoimiliki.

Aidha alisema jirani huyo ametoboa ukuta wake eneo lililoko pembezoni mwa nyumba yake kujenga jiko linalomsababishia kero kubwa, huku viongozi wakubwa wengi wakitembelea kuleta suluhu, lakini kwa miaka yote hiyo hakuna linalofanyika .

# Waziri aridhishwa utendaji mamlaka viwanja vya ndege

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk Khalid Mohamed, ameridhishwa na hatua zinazochukuliwa na watendaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege katika kuimarisha mazingira bora ya uwanja na ya utoaji wa huduma.

Waziri Dk. Khalid alieleza hayo alipokuwa katika mwendelezo wa ziara zake pamoja na naibu waziri wa wizara hiyo ya kukagua maeneo mbalimbali kwa lengo la kuzitambua taasisi zinazounda Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

Alisema ameridhishwa na jitihada zinazochukuliwa na watendaji wa mamlaka hiyo hasa katika harakati za ujenzi katika kuipatia ufumbuzi changamoto ya kuondosha maji katika uwanja huo.

Waziri huyo pia alieleza pamoja na jitihada nzuri zinazochukuliwa na watendaji wa mamlaka ya viwanja vya ndege lakini ameshauri kuchukuliwa kwa hatua za makusudi za kuhamishia shughuli za ushushaji wa abiria kwenye jengo namba 3 la abiria ili kuondosha changamoto ya msongamano kwenye jengo nambari 2.

Pia, katika ziara hiyo, viongozi hao walipata fursa ya kutembelea maeneo yaliyoainishwa kutumiwa na mamlaka ya viwanja vya ndege ambayo kwa sasa baadhi ya maeneo hayo yanakaliwa na wananchi.

Akizungumzia juu ya maeneo hayo Waziri huyo alieleza kuwa, lengo la kufanya ziara katika maeneo hayo ni kuangalia hatua zinazoendelea ambapo amewataka wananchi kutokuwa na taharuki na serikali inaendelea na mchakato wa mipango yake juu ya maeneo hayo na baada ya kukamilika kwa mipango hiyo wananchi watapewa taarifa kamili.

“Nawaomba wananchi wanaoishi katika maeneo ya karibu ambayo yamewekwa alama wasiwe na hofu na ziara hii, ziara hii hailengi kuchukua hatua yoyote,” alifafanua Dk. Khalid.

Katika hatua nyingine, waziri huyo aliwashauri viongozi na watendaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuwa na mikakati ya muda mrefu inayofafanua dhamira na dira ya mamlaka ili kutoa urahisi katika utekelezaji wake.

Naye, Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar,

Seif Abdalla Juma, alisema kupitia ziara ya viongozi hao wa Wizara Mamlaka hiyo itayafanyia kazi mapendekezo na maoni yote yaliotolewa ili kuufanya Uwanja wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume kuendelea kutoa huduma bora kitaifa na Kimataifa.

Ziara hizo za viongozi wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi zinalenga kuimarisha utendaji kazi wa taasisi na idara tofauti zilizomo ndani ya Wizara hiyo.




Mwanafunzi wa Taasisi ya Karume Sayansi na Teknolojia Zanzibar (KIST), Abdulatif Omar (kushoto), akitoa maelezo kwa waratibu wa mashindano ya sayansi na ubunifu, kuhusu mfumo wa kujaza maji kwenye matangi kwa kutumia mashine na kujizima yenyewe yanapojaa, walipotembelea kukagua ubunifu uliofanywa na wanafunzi wa taasisi hiyo, Mbweni Mjini Zanzibar, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Makandarasi watakiwa kusimamia mikataba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKANDARASI wa miradi ya maendeleo wametakiwa kusimamia mikataba waliyofunga na wizara husika ili kuikamilisha kwa wakati uliopangwa.

Kauli hiyo ilitolewa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, katika ziara ya kukagua miradi inayojengwa kwa fedha za mkopo wa ahueni ya UVIKO-19 katika Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alieleza kutoridhishwa kwake kwa baadhi ya makandarasi walio nje ya muda ambao wanasababisha kuchelewa kukamilika kwa miradi hiyo.

Hemed alieleza kuwa masharti ya fedha hizo ifikapo mwezi wa sita mwaka huu ziwe zimeshatumika katika miradi mbalimbali ambapo kwa umuhimu wake serikali imeelekeza fedha hizo zitumike katika sekta za jamii.

Hata hivyo, Makamu wa Pili amesikitishwa na baadhi ya watendaji wa Wilaya na Halmashauri kutoshirikiana kwa pamoja katika kusimamia na kufuatilia miradi hiyo jambo ambalo serikali imekwisha elekeza viongozi hao kuwa karibu na makandarasi waliokabidhiwa miradi hiyo.

Kadhalika, Hemed ameuagiza uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kuajiri Mshauri elekezi ili kusimamia ubora wa majengo hayo.

Aidha, ameutaka uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha wanatatua changamoto ya upatikanaji wa mabati ili kukamilisha ujenzi wa madarasa ambayo asilimia kubwa yamefikia hatua ya uezekaji.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Muhamed Mahmoud, alisema kuwa katika mgawo wa ujenzi wa madarasa mkoa huo umebahatika kupata madarasa 188 pamoja na vyoo na kueleza kuwa kukamilika kwa madarasa hayo kutapunguza changamoto ya uhaba wa madarasa kwa wanafunzi wa mkoa huo.

Aidha Ayoub aliahidi kusimamia miradi yote iliyomo katika mkoa huo kumalizika kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa na kusema kuwa serikali ya mkoa itasimamia maagizo yote yaliyotolewa na serikali kuu.

Kamishna wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar, Khamis Bakar Khamis, alisema kuwa ujenzi unaendelea vyema chini ya ukandarasi wa Chuo hicho na kuahidi majengo ya Mkwajuni na mengineyo kukamilika kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

FOMU MIRATHI - 2

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi Na. 679/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU MOHAMED JAMA YUSUF**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA**
**NA ZAHRA ELMI JAMA**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 5 Mwezi 05 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakama kukaguliwa.

**Imetolewa leo tarehe 05 Mwezi 04 Mwaka 2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKEkituo cha JUMUISHI mkoa DAR ES SALAAM usimamizi wa mirathi No. 680/2022**
**Katika shauri la mirathi ya**
**Marehemu TWAHA ATHUMANI SHEKASHIHA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA**
**SELEMANI ATHUMANI RAMADHANI**

**TANGAZO**

(KANUNI YA 5(2) YA KANUNI ZA USIMAMIZI WA MIRATHI MAHAKAMA ZA MWANZO)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 21 mwezi 04 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

**Zingatia,** endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa

Imetolewa leo tarehe 05/04/2022

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

ROSEMIN JUSAB VIRJI anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T299BRX aina ya TOYOTA ACN10. Chassis No. ACN100004299, Engine No.1AZ4023393.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/134116/2022.

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**UMMYKULTHUM KHATIBU** ANATANGAZA KUPOTEA KWA CHETI CHA DEGREE YA UHASIBU KILICHOTOLEWA NA CHUO CHA TUMAINI UNIVERSITY MAKUMIRA MWAKA **2012** CHENYE NAMBA YA USAJILI **TU/SMMUCo/09/393.** KWA YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI-
ARU/ARU/RB /129365/2022.

---

## TANGAZO LA KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

**FINEHASI MBORA LEMA** anatangaza kupotelewa na Ofa ya kiwanja **Plot Namba 966 Kitalu "H"** kilichopo **Mbezi Dar es salaam** kwa jina la **LAWRENCE J. KIBARU.** Kwa yeyoye atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya Polisi:
**DAR/URA/RB/349789/2021.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

MAHAMOUD WALII ALLY anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili T453CJA, CHASSIS NAMBA TD01W212422, ENGINE NAMBA: G16A562389. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/90400/2022

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOHAMED RASHID MIKIDADI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 727 DCN** aina ya **SUZUKI ESCUDO,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**ARU/ARU/RB/139627/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKEkituo cha JUMUISHI mkoa DAR ES SALAAM usimamizi wa mirathi nan 680/2022**
**Katika shauri la mirathi ya**
**Marehemu TWAHA ATHUMANI SHEKASHIHA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SELEMANI ATHUMANI RAMADHANI**

**TANGAZO**

**(KANUNI YA 5(2) YA KANUNI ZA USIMAMIZI WA MIRATHI MAHAKAMA ZA MWANZO)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 21 mwezi 04 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

**Zingatia,** endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa

**Imetolewa leo tarehe 05/04/2022**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**LOY LUCAS** anatangaza kupotea kwa cheti .cha kidato cha nne chenye **INDEX NAMBA S1633/0118** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya Sekondari **OLD TANGA mwaka 2007.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: LUS/RB/372/2015**

---

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Rais Compaoré afungwa jela maisha

**Ouagadougou,** BURIKA FASO

Rais wa zamani wa Burkina Faso, Blaise Compaore amehukumiwa kifungo cha maisha jela, kwa kushiriki katika mauaji ya mtangulizi wake Thomas Sankara.

Sankara aliuawa akiwa pamoja na wasaidizi wake 12 wakati wa mapinduzi ya mwaka 1987.

Mahakama ya Kijeshi ya Ouagadougou pia imemhukumu kifungo cha maisha jela Kamanda wa Kikosi cha Ulinzi, Hyacinthe Kafando na Jenerali Gilbert Diendere, mmoja wa viongozi wa jeshi wakati wa mapinduzi ya mwaka 1987.

Blaise Compaore, ambaye yuko uhamishoni tangu mwaka 2014 nchini Ivory Coast na Hyacinthe Kafando, ambaye yuko mafichoni tangu mwaka 2016, hawakuhudhuria kesi hiyo iliyoanza miezi sita iliyopita.

Ilichukua miaka kadhaa ya uchunguzi, kesi ambayo walihusishwa mashahidi zaidi ya 110 na kesi hiyo imesikilizwa kwa miezi sita hadi kufikia jana.

UCHAGUZI MKUU KENYA

# Kambi ya Odinga yateua mkurugenzi

**Nairobi,** KENYA

RAPHAEL Tuju ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Sekretarieti Muungano wa Vyama linalojulikana Azimio la Umoja One Kenya, kiongozi wake Raila Odinga alitangaza, jana.

Tuju, aliyekuwa Katibu Mkuu wa chama cha Jubilee ataratibu vyama wanachama na anakuwa mkuu wa mikakati na shughuli za programu katika sekretarieti.

"Ataongoza timu za mikakati na programu ambazo zitafanya kazi kuhakikisha Azimio inashinda katika uchaguzi wa Agosti," Msemaji wa Odinga, Dennis Onyango alisema kwenye taarifa yake.

Muungano huo, unaleta pamoja zaidi ya vyama 20 vya kisiasa kikiwamo chama tawala cha Jubilee kinachoongozwa na Rais Uhuru Kenyatta, ODM cha Odinga na Wiper, inayoongozwa na Kalonzo Musyoka.

• **Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao**



Rais wa zamani Burkina Faso, Blaise Compaore. **PICHA: DW**

MASHAMBULIZI RUSSIA-UKRAINE:

# UN 'yabariki' uchunguzi vifo kwenye mji wa Bucha

**Kyiv,** UKRAINE

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres ametoa wito wa kimataifa kutaka uchunguzi wa madai ya uhalifu wa kivita kutokana na mauaji ya raia kwenye mji wa Bucha nchini Ukraine.

Maoni ya Katibu Mkuu yanakuja baada ya picha kutoka mji wa Bucha, ulioko viunga vya mji mkuu wa Ukraine, Kyiv, kuonyesha miili ya mamia ya watu.

Guterres ambaye alikuwa anahutubia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, alisema uchunguzi huru unahitajika ili uwajibikaji uweze kuwa wa uhakika.

Alisema, Ukraine ni moja ya changamoto kubwa zaidi kuwahi kukabili mfumo wa kimataifa na muundo wa amani duniani ulioasisiwa na Chata ya Umoja wa Mataifa.

"Hadi jana , mashambulizi ya Russia yamesababisha watu zaidi ya milioni 10 kufurushwa makwao ikiwa ni idadi kubwa zaidi tangu Vita Kuu ya Pili ya Dunia," alisema Katibu Mkuu.

Miongoni mwao hao, zaidi ya milioni 4.2 wamevuka mpaka wa Ukraine na kukimbilia nchi jirani, limesema shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi, UNHCR.

Nalo Shirika la Umoja wa Mataifa la Afya Duniani (WHO), linasema mashambulizi yasiyochagua maeneo yameharibu vituo vya afya 86 kati ya tarehe 24 mwezi Februari hadi 2 mwezi huu.

Kwa kuzingatia hali ya udharura wa sasa, Katibu Mkuu alisema amemuagiza Mratibu wa Umoja wa Mataifa wa misaada ya dharura, Martin Griffiths kusafiri hadi Russia na Ukraine kushinikisha sitisho la haraka la mapigano kwa misingi ya kibinadamu.

Msalaba Mwekundu jana ulifanya uhamishaji wa watu 500 kutoka mji wa bandari wa Mariupol uliozingirwa Kusini-Mashariki hadi Zaporizhzhia.

Marekani na Jumuiya ya Ulaya (EU), wako tayari kuiwekea Russia vikwazo zaidi huku kukiwa na madai ya uhalifu wa kivita katika mji wa Bucha

Washington inaripotiwa kuangalia uwezekano wa kuchukua hatua zinazowalenga mabinti wawili wa Rais Putin na benki kubwa zaidi ya Russia.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky aliyetoa hotuba kwa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, aliainisha orodha ya maafa yanayodaiwa kufanywa na Warusi.

Katika kauli kali ambayo haijawahi kutolewa tangu ilipovamiwa.

India imelaani mauaji katika mji wa Bucha nchini Ukraine na kuunga mkono miito ya kufanyika kwa uchunguzi huru juu ya ripoti zinazosikitisha sana.

Vikosi vya Russia vimelenga juhudi zake operesheni ya uchokozi inayolenga kupata udhibiti kamili wa majimbo ya Donetsk na Luhansk.

Mkuu wa Majeshi ya Ukraine alisema katika taarifa za kila siku kuhusu mzozo wa Ukraine.

Mapigano makali na mashambulio ya ndege za Russia, yameendelea katika mji wa mwambao wa Mariupol, kulingana na taarifa za hivi punde za ujasusi kutoka Wizara ya Ulinzi ya Uingereza.

Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Nato, watakutana mjini Brussels, kwa ajili ya mazungumzo ya siku mbili kujadili njia bora zaidi ya kuisaidia Ukraine katika awamu ijayo ya mzozo.

Marekani imetangaza kuwa imeipatia Ukraine silaha nyingine zenye thamani ya Dola milioni 100.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken alisema msaada huo utakidhi mahitaji ya dharura ya silaha za kushambulia ikiwamo vifaru na magari ya kijeshi.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Marekani iliidhinisha dola milioni 300 za silaha kwa ajili ya Ukraine.

Miongoni mwa mambo mengine, fedha hizo zinalenga kufadhili ununuzi wa ndege zisizotumia rubani, pamoja na mifumo ya makombora na magari ya kivita, risasi na vifaa vya kuona usiku.

Kiasi hicho kinafikisha jumla ya msaada wa Marekani kwa Ukraine kuwa dola bilioni 1.7 kwa mujibu wa Wizara ya Ulinzi, Pentagon.

Vikosi vya Russia, kwa sasa vinadhibiti eneo kubwa la Luhansk na zaidi ya nusu ya Donetsk, huku vikijaribu kulizingira jeshi la Ukraine.

Inadaiwa kuwa Russia inaendelea kutumia kikamilifu risasi zilizopigwa marufuku na sheria za kimataifa.

# NBC NA 'JAZA KIBUBU TUSEPE' SIMBA, YANGA, KOMBE LA DUNIA

**Na Jumanne Juma**

BENKI ya NBC imezindua Kampeni ya 'Jaza Kibubu Tusepe', itakayojikita katika utoaji wa elimu kwenye masuala ya kifedha huku ikiambatana na zawadi chungu nzima kwa wateja wake zikiwamo pia tiketi 80 za bure za kushuhudia mechi ya watani wa jadi Simba na Yanga, Aprili 30, mwaka huu pamoja na Kombe la Dunia Qatar.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Bidhaa na Mauzo kwa Wateja Binafsi, Abel Kaseko, alisema kuwa kampeni hiyo itakuwa ya miezi sita na kwamba wateja wa NBC watanufaika vilivyo na kampeni hiyo.

Kaseko alisema kuwa kampeni hiyo itadumu kwa muda wa miezi sita na kwamba elimu itatolewa sambamba na zawadi huku wateja 80 wa benki hiyo wakijishindia tiketi za kushuhudia mchezo wa watani wa Jadi Simba na Yanga utakaochezwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Aprili 30, mwaka huu.

Akifafanua namna ya kushiriki kampeni hiyo, Meneja wa Bidhaa kwa Wateja Binafsi wa beki hiyo, Dorothea Mabonye, alisema mteja atakayeweka kiasi cha Sh. 300,000 kwa kudunduliza kuanzia jana, Aprili 6 hadi Aprili 24, mwaka huu atapata nafasi ya kushinda tiketi ya kushuhudi mchezo huo wa watani wa jadi.

Alisema wateja 50 kutoka mikoa mbalimbali nchini watazawadiwa tiketi za kushuhudia mtanange huo huku wakigharamiwa chakula na malazi wakiwa Dar es Salaam.

**Aidha, Mabonye alisema kuwa wateja 30 kutoka Dar es Salaam kila mmoja atazawadiwa tiketi ya VIP kwenye mchezo huo.**

Mbali na zawadi hiyo, Mabonye alisema kutakuwa na tiketi za washindi watano wa safari ya kushuhudia fainali za Kombe la Dunia nchini Qatar baadaye mwaka huu.

Akifafanua kuhusu upande wa washindi wa Kombe la Dunia, alisema kutakuwa na kundi la mwanzo la washindi wa safari hiyo ambao watadunduliza kwenye akaunti zao za NBC kiasi cha Sh. milioni moja kuanzia jana Aprili 6 mpaka Septamba mwaka huu.

"Kundi la pili litawahusu wateja wetu watakaoweka kwa kudunduliza kiasi cha Sh. 7,000,000 kwenye akaunti zao kuanzia Aprili 6 mpaka Septemba, kundi hili litakuwa linawashindi wawili watakaozawadiwa tiketi za safari ya Qatar, malazi, vyakula na vinywaji na kushuhudia mechi kwenye fainali za Kombe la Dunia. Hawa watapata tiketi za mzunguko,"alisema Mabonye huku akitoa wito kwa Watanzania kufungua akaunti kwenye benki hiyo ili kunufaika na kampeni hiyo.



Mkuu wa Kitengo cha Mawakala wa Benki ya NBC, Gaudence Showa(kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana wakati wa uzinduzi wa Kampeni ya Jaza Kibubu Tusepe, inayolenga kutoa zawadi kibao kwa wateja wake ikiwamo kuwalipia tiketi 80 kwenda kushuhudia mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga Aprili 30, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na wengine Kombe la Dunia nchini Qatar. Katikati ni Mkuu wa Kitengo cha Bidhaa na Mauzo wa benki hiyo, Abel Kaseko na kulia ni Meneja Bidhaa na Mauzo, Dorothea Mabonye. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Djuma akerwa pasi za nyuma

**Dennis Fussi na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Dodoma Jiji, Masoud Djuma, amesema anakwenda kulifanyia kazi tatizo la wachezaji wake kupenda kurudisha mipira nyuma, kitu ambacho kinawagharimu na kufungwa mabao mepesi.

Kocha huyo raia wa Burundi, amesema kumekuwa na makosa ya wachezaji wake kupenda kurudisha pasi nyuma mara kwa mara bila sababu yoyote, hivyo ameamua kulivalia njuga suala hilo.

"Hata mabao tuliyofungwa na Prisons, kwa kupoteza 3-2 Jumatatu, yalikuwa ya aina hiyo, kuna wakati wachezaji wanarudisha mpira nyuma bila sababu yoyote ya msingi, mipira inakutana na wapinzani wanakwenda kutuadhibu, lakini tuanze kulifanyia kazi hili," alisema kocha huyo wa zamani wa Simba.

Ikiwa inaongoza 2-1 hadi dakika ya 77, Dodoma Jiji ilijikuta ikifungwa mabao mawili ya haraka na hadi filimbi ya mwisho inapulizwa, ubao ulikuwa unasomeka 3-2.

Masoud alichukua kijiti cha kuifundisha timu hiyo Februari mwaka huu, kutoka kwa kocha Mbwana Makata, ambaye naye kwa sasa amekwenda anakinoa kikosi cha Mbeya Kwanza FC.

Katika hatua nyingine Djuma amewataka wachezaji wake kuongeza umakini, ili kuendana na ushindani uliopo kwenye ligi.

Kocha huyo alisema wameshindwa kupata ushindi katika mechi mbili zilizopita kutokana na uzembe wa safu yake ya ulinzi, kitu ambacho kimewagharimu na kujikuta wakipoteza.

"Nina timu nzuri ambayo inashika haraka kile ninachowapa, lakini tatizo lao wanapoteza umakini, jambo ambalo linatugharimu na kujikuta tunapoteza mchezo, ukizingatia timu ipo kwenye nafasi mbaya na ligi ndio inazidi kusonga mbele," alisema Djuma.

Timu hiyo inashika nafasi ya 12 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwa imevuna pointi 21 kwenye mechi 19 ambazo imecheza hadi sasa.

# *BMT na ufafanuzi matumizi rasilimali mfuko wa michezo*

**Na Saada Akida**

KATIBU Mtendaji wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Neema Msitha, amesema matumizi ya rasilimali za mfuko wa maendeleo ya michezo yatafuata sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya matumizi ya fedha za serikali inavyotolewa kila mwaka wa fedha wa serikali.

Msitha alisema hayo wakati akiwasilisha mada kuhusu kuundwa kwa mfuko wa maendeleo ya michezo unaotokana na michezo ya kubashiri, unaosimamiwa na BMT.

Alisema mfuko huo upo kwa ajili ya maendeleo ya michezo na matumizi ya fedha hizo yatafanyika kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya matumizi ya fedha za serikali inayotolewa kila mwaka wa fedha.

"Majukumu ya mfuko huo ni kuwezesha kukuza maendeleo ya michezo kwa kutafuta na kupokea fedha kutoka vyanzo mbalimbali kugharamia shughuli za michezo," alisema na aliongeza;

"Kugharamia timu za taifa na wanamichezo wanaoiwakilisha nchi katika mashindano ya kimataifa, kugharamia ujenzi, matengenezo ya miundombinu ya michezo na ununuzi wa vifaa na zana za michezo."

Alisema fedha hizo pia zitagharamia mafunzo kwa wanamichezo, kuwezesha wizara yenye dhamana ya michezo na kutekeleza majukumu yanayohusiana na maendeleo ya michezo.

Alisema mengine ni pamoja na kukuza afya za Watanzania, kuwezesha ukuaji wa masoko, ukuzaji wa vipaji, matangazo, harambee na matukio ya kitaifa na kimataifa ya michezo na kuwezesha dhana ya utawala bora katika michezo.

"Vipaumbele vya mfuko ni kusaidia timu za taifa, kusaidia ujenzi wa miundombinu ya michezo, vifaa vya michezo na kuwezesha mafunzo kwa wataalamu wa michezo na wanamichezo," alisema Neema Msitha.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### POGBA APEWA OFA PSG
KLABU ya Paris St-Germain imetoa ofa kwa kiungo wa kati wa Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 29, wakati huu akiingia miezi ya mwisho ya mkataba wake na Manchester United. (***MEN***)

### KANE KUSIKILIZIA
MSHAMBULIAJI wa Tottenham na England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 28, atakuwa na hamu ya kutaka kusikiliza ofa yoyote kutoka kwa Manchester United msimu huu wa majira ya joto kabla ya kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wake. (***The Athletic***)

### ZAHA KUPIGWA BEI
KLABU ya Crystal Palace itasikiliza ofa kwa mshambuliaji wa Ivory Coast, Wilfried Zaha mwenye umri wa miaka 29.(***Mail***)

### MADRID UHAKIKA KWA MBAPPE
REAL Madrid wana uhakika wa kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 23, kutoka PSG msimu huu wa majira ya joto, licha ya ripoti kuonyesha kuwa anakaribia kukubali mkataba mpya wa kubakia Paris. (***90min***)

### BALE KUONDOKA MADRID
MSHAMBULIAJI wa Wales, Gareth Bale mwenye umri wa miaka 32, ataondoka Real Madrid mwishoni mwa msimu huu, lakini hakuna uamuzi wowote ambao umefanywa kuhusu hatma yake ya baadaye, wakala wake amesema. (***Deportes Cuatro, via Mirror***)

### NUNEZ AWINDWA UNITED
MANCHESTER United na Atletico Madrid ni miongoni mwa timu kadhaa zinazofikiria kumnunua mshambuliaji wa Benfica raia wa Uruguay, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 22. (***Telegraph***)

### LIVERPOOL KUSAJILI WATATU
LIVERPOOL wanakaribia kusajili wachezaji watatu wapya. 'Wekundu' hao wamefikia makubaliano ya kuwachukua kiungo wa kati wa Fulham, Fabio Carvalho mwenye umri wa miaka 19, winga wa Celtic raia wa Scotland, Ben Doak mwenye miaka 16, na winga wa Derry City,Trent Kone-Doherty mwenye miaka 15. (***Football Insider***)

### FODEN KUPEWA MKATABA
MANCHESTER City wana matumaini ya kumpa mkataba mpya na kiungo wa kati wa England, Phil Foden mwenye umri wa miaka 21, kabla ya mwishoni mwa msimu huu. (***90min***)

### HAG KUONDOKA NA NYOTA
UTEUZI unaowezekana wa Erik ten Hag kama kocha mpya wa Manchester United unaweza kumfanya mlinzi wa Uholanzi, Jurrien Timber mwenye umri wa miaka 22, na winga wa Brazil Antony, 22, kumfuata kutoka Ajax msimu huu wa majira ya joto. (***Mike Verweij, via Express***)

### RANGNICK KUMLETA LAIMER
KOCHA wa muda wa Manchester United, Ralf Rangnick anaweza kutumia fursa ya mawasiliano yake na RB Leipzig kumleta kiungo wa kati wa Austria, Konrad Laimer mwenye umri wa miaka 24, Old Trafford. (***Bild, via Express***)

### SAINT-MAXIMIN KUUZWA
NEWCASTLE United wako tayari kumuuza mshambuliaji, Allan Saint-Maximin mwenye umri wa miaka 25 msimu huu wa majira taa joto. (***90min***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# DE BRUYNE ATOA SIRI YA USHINDI ATLETICO

**Unahitaji kuwa mtulivu, mvumilivu, na kujaribu kutafuta nafasi, lakini tulipata nafasi kadhaa katika kipindi cha pili...**

**MANCHESTER,** ENGLAND

KEVIN De Bruyne anaamini kuwa Manchester City walizawadiwa kwa utulivu na subira wakati wa mechi ya robo fainali ya mkondo wa kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya waliposhinda bao 1-0 dhidi ya Atletico Madrid, Jumanne.

De Bruyne alifikisha mechi yake ya 50 kwa Man City katika kinyang'anyiro hicho kwa kufunga bao pekee kwenye Uwanja wa Etihad. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji aliutumia mpira mtamu wa Phil Foden dakika 20 kabla ya kumfunga golikipa, Jan Oblak kwa ustadi mkubwa.

City walikuwa na wakati mgumu kwenye mchezo huo, huku wakihangaika kuvunja safu ya ulinzi ya wapinzani wao ambayo ilikuwa ngumu.

**Lakini uvumilivu wao hatimaye ulizaa matunda kwa vijana wa Pep Guardiola kuchukua uongozi mwembamba kwa Atletico Madrid, huku wakisubiri mechi ya marudiano wiki ijayo.**

"Ulikuwa mchezo mgumu sana," alisema De Bruyne akiiambia BT Sport baada ya mchezo huo.

"Wanacheza kwa ulinzi mkali na imara; hiyo ndiyo njia yao ya kucheza. Nadhani tulicheza vizuri chini ya mazingira.

"Walicheza karibu watano nyuma na watano katikati, kwa hivyo ni ngumu sana kupata nafasi.

"Unahitaji kuwa mtulivu, mvumilivu, na kujaribu kutafuta nafasi. Lakini tulipata nafasi kadhaa katika kipindi cha pili na tukafanikiwa kupata moja.

"Natarajia vivyo hivyo huko (katika mchezo wa pili). Ikiwa mchezo utakuwa mkali, watalazimika kushambulia zaidi."

Vijana wa Diego Simeone walisili Manchester kwa mara ya pili ndani ya mwezi mmoja - baada ya kuwashinda United katika Uwanja wa Old Trafford katika raundi ya awali.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT
TZS. 1,119

MECHI KALI
COASTAL UNION
VERSUS
SIMBA
1 | 6.23
X | 3.31
2 | 1.57

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# BARCA WAJIPANGA KUMSAJILI RAPHINHA

**BARCELONA,** Hispania

MAZUNGUMZO yameanza kuhusu uwezekano wa Raphinha kuhama kutoka Leeds United kwenda Barcelona, kwa mujibu wa mwandishi wa habari za michezo wa Italia, Nicolo Schira.

Tangu ujio wa Xavi kule Barcelona kumekuwa na ujenzi mpya wa kikosi hicho ambacho sasa kipo nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga. Klabu iliyoripotiwa kutumia euro milioni 275 kwa jumla kuwanunua Ousmane Dembele na Philippe Coutinho, sasa inawinda winga mpya, na Raphinha anaonekana kukidhi vigezo.

Wakala wa Raphinha, nyota wa zamani wa Barcelona na Chelsea, Deco, amekuwa akiwasiliana na wababe hao wa Katalunya tangu Machi, lakini kipengele cha kutolewa kwa winga huyo wa Brazil kwa euro milioni 70 kimekuwa kikwazo kwa klabu hiyo yenye uhaba wa fedha.

Mchezaji mwenye umri wa miaka 25, ameonyesha nia ya wazi ya kutaka kujiunga na 'Blaugrana' hao, ambapo amefikisha mabao tisa na kutoa pasi tatu za mabao katika mechi 28 akiwa na Leeds.

Inaarifiwa Barcelona itajaribu kuja na ofa itakayokubalika kwa klabu hiyo ya Ligi Kuu England katika wiki ijayo.



# Klopp: Liverpool kwa mbinde

**LISBON,** Ureno

JURGEN Klopp amefichua kwamba, hakutarajia zaidi ya ugumu mkubwa walioupata Liverpool wakati wakipata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Benfica, Jumanne.

'Wekundu' hao walichukua udhibiti wa mchezo wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa ushindi nchini Ureno, lakini mchezo haukuwa wa kustarehesha kama ambavyo matokeo yanavyoonyesha.

Wenyeji walionekana kuwa wagumu baada ya Darwin Nunez kupunguza nusu ya bao mapema katika kipindi cha pili na walikuwa na bahati mbaya ya kuruhusu bao la Luis Diaz.

Hata hivyo, changamoto iliyoletwa na Benfica hakika haikumshangaza kocha Klopp, ambaye alisema: "Mwishowe, kuja hapa katika mchezo wa ugenini katika Ligi ya Mabingwa Ulaya ni ngumu. Ni wazi, Benfica walipigania maisha yao.

"Tulifungua mlango kidogo sana, lakini walistahili bao pia, hata wakati tungeweza kujilinda vizuri zaidi. Si kwamba hapo awali hakukuwa na hali yoyote.

"Ulikuwa mchezo mgumu, nilichotarajia hasa walipofunga, tulijua, tunajua siku zote, 2-0 si kitu, ni nzuri lakini si zaidi.

,012,860

# JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 09/04/22 | 17:00 | Watford vs Leeds | 2.75 | 3.29 | 2.49 |
| 02. 09/04/22 | 17:00 | Preston vs QPR | 2.48 | 3.17 | 2.77 |
| 03. 09/04/22 | 17:00 | Bolton vs Sheffield Wed | 2.63 | 3.13 | 2.63 |
| 04. 09/04/22 | 19:30 | Hertha BSC vs Union Berlin | 2.69 | 3.19 | 2.59 |
| 05. 09/04/22 | 20:00 | Amiens vs Bastia | 2.63 | 2.93 | 2.78 |
| 06. 10/04/22 | 15:15 | Servette Geneva vs FC Zurich | 2.37 | 3.48 | 2.73 |
| 07. 10/04/22 | 16:00 | Sivasspor vs Basaksehir | 2.50 | 3.30 | 2.70 |
| 08. 10/04/22 | 16:00 | Brentford vs West Ham | 2.70 | 3.25 | 2.55 |
| 09. 10/04/22 | 16:00 | Norwich City vs Burnley | 2.75 | 3.10 | 2.60 |
| 10. 10/04/22 | 16:00 | Brest vs Nantes | 2.43 | 3.22 | 2.92 |
| 11. 10/04/22 | 17:15 | Espanyol vs Celta Vigo | 2.78 | 3.13 | 2.63 |
| 12. 10/04/22 | 17:30 | St. Gallen vs FC Basel | 2.39 | 3.53 | 2.68 |
| 13. 10/04/22 | 20:00 | Strasbourg vs Lyon | 2.60 | 3.30 | 2.65 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 07/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4739 | Istanbulspor U19 vs Bursaspor U19 | 3.59 | 3.74 | 1.81 |
| 13:30 | 2386 | Bashundhara Kings vs Sheikh Jamal | 1.80 | 3.50 | 3.88 |
| 14:00 | 4155 | Lernayin Artsakh vs Ararat Armenia II | 1.17 | 6.45 | 10.76 |
| 14:00 | 5315 | Artsakh vs Van Yerevan | 1.63 | 3.45 | 5.05 |
| 15:00 | 2624 | Dire Dawa Kenema FC vs Sidama Bunna SC | 6.03 | 3.89 | 1.48 |
| 15:30 | 2122 | Kalaa Sport vs AS Djerba | 2.04 | 2.92 | 3.75 |
| 15:30 | 5582 | EO Sidi Bouzid vs Avenir Sportif Gabesien | 2.34 | 2.73 | 3.27 |
| 16:00 | 3217 | Coastal Union vs Simba | 6.23 | 3.31 | 1.57 |
| 16:00 | 4585 | Kafue Celtic FC vs Zanaco | 2.86 | 2.62 | 2.71 |
| 17:00 | 1425 | Atlas U20 vs Necaxa U20 | 1.95 | 3.56 | 3.27 |
| 17:00 | 2529 | Jeugd Rfc Seraing United U21 vs Lierse SK | 1.93 | 3.56 | 3.32 |
| 17:00 | 4281 | Nitra U19 vs Slovan Bratislava U19 | 7.19 | 5.05 | 1.31 |
| 17:00 | 4811 | Pachuca U20 vs Tigres U20 | 2.07 | 3.40 | 3.11 |
| 17:30 | 4024 | SK Super Nova vs FK Tukums 2000/Tss | 2.61 | 3.29 | 2.42 |
| 17:45 | 5993 | Ol. Medea vs CR Belouizdad | 4.48 | 2.68 | 1.99 |
| 18:00 | 1670 | Arba Minch Kenema vs Addis Ababa City FC | 2.48 | 2.80 | 3.20 |
| 18:00 | 4679 | Honka vs Haka | 2.11 | 3.05 | 3.34 |
| 19:00 | 1803 | Georgia W vs Sweden W | 27.27 | 21.43 | 1.01 |
| 19:00 | 2097 | Skra Czestochowa vs Chrobry Glogow | 3.22 | 3.02 | 2.18 |
| 19:30 | 5915 | Universitatea Cluj vs CSA Steaua Bucuresti | 2.01 | 3.12 | 3.56 |
| 19:45 | 3069 | RB Leipzig vs Atalanta | 1.84 | 3.79 | 3.95 |
| 19:45 | 5822 | Hvidovre IF vs Lyngby | 2.97 | 3.36 | 2.14 |
| 19:45 | 5919 | Feyenoord vs Slavia Prague | 1.70 | 3.99 | 4.54 |
| 20:30 | 1058 | Al Seeb vs Sohar Club | 1.33 | 4.37 | 8.35 |
| 20:30 | 1496 | FC Gutersloh vs TSG Sprockhovel | 1.53 | 4.29 | 4.68 |
| 20:30 | 1697 | Holzwickeder SC vs 1. FC Kaan-Marienborn | 10.64 | 6.58 | 1.17 |
| 20:30 | 1698 | TUS Ennepetal vs RSV Meinerzhagen | 1.61 | 4.29 | 4.09 |
| 20:30 | 3156 | Varbergs Gif FK vs Ullareds IK | 1.90 | 3.66 | 3.32 |
| 20:30 | 3370 | Anderlecht U21 vs KRC Genk U21 | 2.06 | 3.36 | 3.17 |
| 20:30 | 4057 | Siegen vs SPVGG Vreden 1921 | 1.80 | 4.10 | 3.70 |
| 20:30 | 4090 | SC Preussen Munster II vs SV Schermbeck 1912 | 2.49 | 4.20 | 2.33 |
| 20:30 | 4221 | Nizwa vs Oman Club | 3.69 | 2.91 | 2.06 |
| 20:30 | 4490 | Al Nahda (Oman) vs AL Etihad | 1.56 | 3.54 | 5.63 |
| 20:30 | 5892 | Saham Club vs Bahla | 3.07 | 2.82 | 2.38 |
| 20:45 | 1065 | AS Trencin vs Slovan Bratislava | 4.11 | 3.91 | 1.66 |
| 21:00 | 2087 | VfL Vichttal vs Bergisch Gladbach | 6.61 | 5.05 | 1.33 |
| 21:30 | 1315 | AL Ittihad Bhr vs Malkiya Club | 2.77 | 3.25 | 2.32 |
| 21:30 | 1782 | GKS Tychy vs Arka Gdynia | 2.72 | 3.11 | 2.43 |
| 21:30 | 2101 | Busaiteen vs Sitra Club | 2.85 | 3.35 | 2.39 |
| 21:30 | 3543 | ISA Town vs Al Ittifaq Bhr | 2.31 | 3.35 | 2.72 |
| 21:45 | 1721 | Glacis United FC vs FCB Magpies | 2.63 | 3.61 | 2.25 |
| 22:00 | 1200 | Sporting Braga vs Rangers | 2.37 | 3.29 | 2.99 |
| 22:00 | 1984 | Shabab AL Amari vs Shabab AL Khaleel | 6.42 | 4.77 | 1.36 |
| 22:00 | 3752 | Eintracht Frankfurt vs Barcelona | 4.35 | 3.87 | 1.75 |
| 22:00 | 3754 | Shabab Alsamu vs Mosaset AL Bireh | 1.97 | 3.50 | 3.26 |
| 22:00 | 4619 | Marseille vs PAOK | 1.43 | 4.45 | 7.48 |
| 22:00 | 4637 | Bodo Glimt vs Roma | 3.62 | 3.67 | 1.95 |
| 22:00 | 5443 | Leicester vs PSV Eindhoven | 2.18 | 3.49 | 3.19 |
| 22:00 | 5510 | West Ham vs Lyon | 2.06 | 3.43 | 3.53 |
| 23:00 | 3244 | Fortaleza (COL) vs Club Cortulua | 2.20 | 3.02 | 3.17 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# SERIKALI YAIPONGEZA SIMBA KUNG'ARA MICHUANO YA CAF

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI imeipongeza Klabu ya Simba kwa kuiwakilisha vema Tanzania katika michuano ya soka barani Afrika msimu huu.

Simba, yenye maskani yake Kariakoo jijini Dar es Salaam, Jumapili iliyopita ilitinga hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika na sasa inajiandaa kwa kibarua cha mechi mbili za nyumbani na ugenini dhidi ya Orlando Pirates ya Afrika Kusini.

Pongezi hizo zilitolewa bungeni jijini hapa jana na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipowasilisha hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi yake kwa mwaka ujao wa fedha.

"Kipekee niipongeze Simba Sports Club kwa kupeperusha bendera ya taifa letu katika mashindano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika. Mwenye macho haambiwi tazama, sote tumeshuhudia wakiendelea kupiga mwingi na kutuwakilisha vema katika medani za kimataifa," Majaliwa alisifu.

Waziri Mkuu pia alitumia fursa hiyo kuzipongeza klabu za soka nchini zinazoshiriki ligi mbalimbali, zikiwamo Ligi Kuu Tanzania Bara (NBC Premier League) na Ligi Kuu Zanzibar (PBZ Premier League).

"Hakika kwa mpira mzuri wanaocheza wanakonga mioyo ya mashabiki wa mchezo wa mpira wa miguu nchini. Niwapongeze pia wachezaji mahiri wa klabu mbalimbali za mpira wa miguu ikiwamo Yanga - Timu ya Wananchi; Simba - Wekundu wa Msimbazi; Namungo - Wauaji wa Kusini; Azam FC- Wazee wa Lambalamba.

"Pia, Biashara United - Wanajeshi wa Mpakani; Dodoma Jiji - Walima Zabibu, Tanzania Prison - Wajelajela na bila kuwasahau Mtibwa Sugar - Wakata Miwa na Kagera Sugar - Wanankurukumbi. Vilevile, nizipongeze klabu za Zanzibar, ikiwamo KMKM, Mlandege, Malindi, Mafunzo na klabu nyinginezo," alisema.

Kwa mchezo wa ngumi, Majaliwa aliwapongeza wanamasumbwi Hassan Mwakinyo, Tonny Rashid, Twaha Kiduku na Ibrahim Class kwa ushindi mnono uliowawezesha kupata mikanda katika mashindano mbalimbali ya kimataifa waliyoshiriki.

"Nitumie fursa hii pia kuzipongeza timu za mpira wa miguu za wanawake kwa ushindi wao katika mashindano mbalimbali ya kimataifa. Kipekee, niwapongeze Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars) kwa kutwaa ubingwa katika mashindano ya COSAFA mwaka 2021.

"Vilevile, niipongeze sana Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Watu Wenye Ulemavu (Tembo Warriors) kwa kufuzu kushiriki mashindano ya dunia yatakayofanyika Oktoba, 2022 Uturuki. Hii ni mara ya kwanza timu ya taifa kushinda na kushiriki moja kwa moja mashindano ya dunia," alisifu.

Alisema kuwa katika mwaka 2021/22, serikali imekamilisha ujenzi wa Mfumo wa Usajili na Usimamizi wa Wasanii na Wadau wa Sanaa na kuboresha mfumo wa usajili kwa njia ya kielektroniki.

Alibainisha kuwa mfumo huo umewezesha wabunifu 485 na kazi zao 2,921 kusajiliwa na serikali imewezesha wasanii wa fani ya muziki ambao kazi zao zimetumika kwenye vituo vya redio na televisheni kupata mirabaha.

Waziri Mkuu alisema kuwa katika mwaka ujao wa fedha (2022/23), serikali itaendelea kujenga mazingira wezeshi kwa wadau wa michezo, sanaa na utamaduni ili kuifanya Tanzania kung'ara katika medani za kimataifa.

Alibainisha kuwa serikali pia itajenga shule maalum 56 za kukuza vipaji vya michezo katika maeneo mbalimbali nchini.



Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2022/23 kwenye Kikao cha Bunge la Bajeti Bungeni jijini Dodoma jana ambapo aliomba Bunge kupitisha Sh. 148,892,553,000 kwa ajili ya ofisi hiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Coastal bila Sopu waipania Simba

**Na Cheji Bakari, Tanga**

WAKATI leo wakiikaribisha Simba kwenye mechi ya raundi ya pili ya Ligi Kuu Bara katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, wenyeji Coastal Union mbali na kupania kuondoka na alama tatu, wametamba kutandaza soka la kiwango na kuvutia.

Katika mchezo wa raundi ya kwanza uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, timu hizo zilitoka suluhu.

Akizungumza na mwandishi wetu jana kuelekea mchezo huo, Msemaji wa Coastal Union, Miraji Wandi, alisema mechi hiyo itakayopigwa majira saa10:00 alasiri si tu wanazitaka alama tatu, bali pia wataonyesha soka la kuvutia.

Wandi alisema licha ya kuwa na majeruhi wawili katika kikosi chao, ambao watakosa mchezo wa leo, lakini wana hazina ya wachezaji wa kutosha na hawaihofii Simba kama inavyotafsiriwa.

"Simba! Labda ungesema timu nyingine zenye saizi yetu ndio timu ngumu kwetu, lakini eti timu kubwa kwamba tuziogope, hiyo hapana, dakika 90 ndizo muamuzi, kikosi chetu kipo vizuri kwa ajili ya mechi hii.

Aliongeza: "Hadi leo (jana) tuna majeruhi wawili, Abdul Hamis " Sopu" na Mtenje Albano lakini tumesajili wachezaji zaidi ya thelathini, nafasi zao zimezibwa hatuna wasiwasi kwa hilo hivyo tuna hazina ya wachezaji".

# Michezo

Alhamisi Aprili 7, 2022

Nipashe




De Bruyne atoa siri ya ushindi Atletico UKURASA 21

# Morrison aitia Simba hasira kwa Orlando

● ● ● Ni wakati akizuiwa kutua Sauzi, kocha raia wa Afrika Kusini amkabidhi Pablo faili...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

KITENDO cha winga Mghana Bernard Morrison, kutoruhusiwa kuingia nchini Afrika Kusini, hivyo kutarajiwa kuikosa mechi ya marudiano ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Orlando Pirates, kimeongeza hasira na ari kwa Klabu ya Simba kupania kumalizia mechi nyumbani.

**Morrison yuko kwenye hatihati ya kutosafiri na timu hiyo kwenye mechi ya marudiano dhidi ya Orlando Pirates Aprili 24, mwaka huu kutokana na kuwa na matatizo kwenye Idara ya Uhamiaji ya Afrika Kusini.**

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, akizungumza na mwandishi wetu jana alisema ni kweli Morrison ana matatizo na idara hiyo, hivyo ni ngumu kuingia nchini Afrika Kusini, lakini kwa sasa wanalishughulikia suala hilo ili wasafiri naye.

"Kuna ukweli, na hili ni bora tuliweke wazi, ni kweli alipata changamoto huko nyuma, unajua ana familia kule, alipata changamoto kwenye idara ya uhamiaji, na hili bado tunaendelea kulitatua, kikubwa ni lazima tufuate sheria za nchi na kusikiliza nini uhamiaji watasema, tukifanikiwa atakwenda na sisi.

"Ndiyo maana shughuli yote tunataka tuimalize tarehe 17 nyumbani Uwanja wa Benjamin Mkapa, ya marudiano iwe ya kumalizia tu," alisema Barbara.

Alisema malengo yao ni kuhakikisha wanapata mabao ya kutosha katika mechi hiyo ya awali nyumbani, katika mchezo wa marudiano kazi iwe kulinda ushindi wao tu.

Barbara aliamua kuweka wazi hilo kutokana na minong'ono ya muda mrefu kuhusu mchezaji huyo kutoruhusiwa kuingia Afrika Kusini, sababu mbalimbali zikitajwa, na hii ni baada ya kutosafiri kwake na timu hiyo ilipokwenda kucheza mechi ya kwanza ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliopita nchini humo iliyochezea Mei 15 mwaka jana dhidi Kaizer Chiefs.

Morrison aliwahi kuishi Sauzi, akiichezea Orlando Pirates msimu wa 2016 hadi 2018, alipotimkia DC Motema Pembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, kabla ya kutua Yanga mwaka 2000, akicheza nusu msimu na kujiunga na Simba.

Wakati huo huo, Kocha wa Makipa wa Simba, Tyron Damons, amesema atakabidhi faili la Orlando Pirates baada mechi zao za Ligi Kuu, kwa kuwa anajua vema timu hiyo ya nchini kwao Afrika Kusini.

Damons ambaye ni raia wa Afrika Kusini amewahi kuziongoza timu kadhaa kucheza dhidi ya Orlando Pirates kwenye Ligi Kuu ya nchini humo, ikiwamo TS Galaxy na Bidvest Wits.

Akizungumzana gazeti hili jana, kocha huyo wa makipa Simba, alisema Orlando Pirates ni timu nzuri lakini ana imani wachezaji wao wakifuata yale wanayopewa mazoezini ana imani kubwa watasonga mbele na kucheza nusu fainali.

"Naifahamu Orlando Pirates, lakini pia tunaweza kupata taarifa zao kutoka Afrika Kusini na baada ya mechi dhidi ya Coastal Union, tutakaa na Kocha Pablo (Franco) kuangalia ubora na udhaifu wa wapinzani wetu," alisema.




Morrison

## Chama, Pablo wawapiku Mayele, Nabi tuzo Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO wa Simba, Clatous Chama amechaguliwa kuwa mchezaji bora wa mwezi Machi, huku Kocha Mkuu wa timu hiyo, Pablo Franco, akiibuka kuwa kocha bora wa mwezi huo wa Ligi Kuu ya Tanzania Bara inayoendelea nchini baada ya wawili hao kuwapiku Fiston Mayele na Nasreddine Nabi wa Yanga.

Taarifa iliyotolewa jana na Bodi ya Ligi, imeeleza kuwa tuzo hizo zimetolewa baada ya kikao cha kamati ya tuzo kilichokutana mwanzoni mwa juma hili.

Ilisema Chama, raia wa Zambia, aliyesajiliwa kwa mara ya pili na Simba akitokea RS Berkane ya Morocco kipindi cha dirisha dogo, alipopigwa bei baada ya kumalizika kwa Ligi Kuu msimu uliopita, amechaguliwa kuwa mchezaji bora wa mwezi uliopita baada ya kuonyesha kiwango kizuri, akisaidia timu yake kupata ushindi kwenye mechi mbili, akifunga pia mabao mawili, akiwapiku Fiston Mayele wa Yanga raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na Mbongo, Frank Kahore wa Mtibwa Sugar.

Chama anakuwa mchezaji wa saba kutwaa tuzo hiyo kwani tayari imeshachukuliwa na wachezaji Mayele mwezi Januari, Saido Ntibazonkiza wa Yanga (Februari) na Feisal Salum pia wa Yanga (Oktoba).

Wengine ni Reliants Lusajo wa Namungo, Desemba, Jeremiah Juma wa Prisons (Novemba), na Vitalius Mayanga wa Polisi Tanzania (Septemba).

Kwa upande wa Pablo, aliwabwaga Mtunisia Nasreddine Nabi wa Yanga na Mkenya Francis Baraza wa Kagera Sugar.

Makocha walioshinda tuzo hiyo mpaka sasa ni Nabi aliyeibeba mara mbili, Februari na Oktoba, Baraza wa Kagera Sugar (Januari), Melis Medo wa Coastal (Desemba), Salum Mayanga wa Tanzania Prisons (Novemba) na Malale Hamsini wa Polisi Tanzania, Septemba.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >